# BUNGE LA TANZANIA

---

## BUNGE LA KUMI NA MBILI

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

### Kikao cha Nne – Tarehe 13 Novemba, 2020

*(Bunge Lilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

*(Saa 3.06 Asubuhi Viongozi wa Kitaifa Walianza Kuingia Ukumbini)*

*Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (Mhe. Zubier Ali Maulid) na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) (Mhe. Martin Ngoga) Waliingia Ukumbini*

*Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma) na Jaji Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (Mhe. Omar Othman Makungu) Waliingia Ukumbini*

*Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi) na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar (Mhe. Hemed Suleiman Abdullah) Waliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge Walipiga Makofi na Vigelegele)*

*Waziri Mkuu Mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa) Aliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge Walipiga Makofi na Vigelegele)*

*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Samia Suluhu Hassan) akiongozana na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Waliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge Walipiga Makofi na Vigelegele)*

*(Saa 3:51 Asubuhi Bunge Lilisitishwa kwa muda)*

*(Saa 4.15 Asubuhi Bunge lilirudia)*

*(Hapa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Dkt. John P. J. Magufuli) akiongozana na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Job Y. Ndugai) Waliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge Walipiga Makofi na Vigelegele)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge, mnaweza kukaa.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais - Mama Samia Suluhu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye amekuwa Mbunge mwenzetu kwa miaka 20 mfululizo humu ndani, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Jaji Mkuu Zanzibar, Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid kutoka Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Spika Martin Ngoga kutoka Bunge la Afrika ya Mashariki ninawakaribisha sana kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, tuna wageni wengi sana kama utakavyoona *galleries* zetu hizo zimejaa, nitawatambulisha

mwishoni baada ya hotuba yako, lakini pia kumbi nyingine za Bunge pia nazo zimejaa wageni nje ya ukumbi huu ambao nao wanafuatilia kila kinachoendelea hapa *live*.

Nichukue nafasi hii kabla sijatoa taarifa yangu rasmi, niseme kwamba Mheshimiwa Rais jumla ya Waheshimiwa Wabunge Kikatiba wa Bunge hili kuwa wanakuwa ni 393 jumla wote, waliopo hivi sasa ni 359. Bado tunasubiri Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Spika upo hapa, bado tunasubiri Wabunge watano hapa. Halafu tunasubiri Mheshimiwa Rais wateule wa kwako kumi; wanawake watano, wanaume watano, pia tunasubiri wale wa Viti Maalum kutoka vyama vingine kwa kadri watakavyokuja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jumla yetu tutakuwa 393 pale tunapokuwa tupo kamili kabisa *full house*, kwa sasa ni 359. Katika hao 359 tuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wabunge wa *CUF* watatu, tunapaswa kuwa na Wabunge wa ACT Wazalendo wanne, tuna Mbunge wa CHADEMA mpaka sasa hivi ni mmoja na tuna Wabunge wa Chama cha Mapinduzi 256.

Mheshimiwa Rais kati ya hao, Wabunge wa Viti Maalum ni 94, lakini wanawake kwa ujumla wanakuwa 94 kujumlisha 24. Ningeomba Wabunge wanawake wote pale mlipo hebu msimame angalau Mheshimiwa Rais apate picha ya uwakilishi wa akina mama Bungeni, kila Mbunge mwanamke asimame, wengine bado wamekaa naomba Wabunge Wanawake wote msimame. *(Makofi/Vigelegele)*

Kwa hiyo, Watanzania wanaweza wakaona uwakilishi wa akina mama ulivyo kwa kweli ni mkubwa kabisa, hongereni sana wote, ni moja ya nchi chache zenye uwakilishi mkubwa kiasi hiki wa wakina mama katika Ukanda wetu wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, pia ningependa niseme kwamba katika Wabunge hawa tulionao hadi hivi sasa, Wabunge wapya kati ya 259 ni 206. Naomba Wabunge wapya msimame pale mlipo, wapya wote. Waandishi wa Habari

picha hii ni muhimu sana ya Wabunge wapya, inatoa picha ya demokrasia ya nchi yetu jinsi ambavyo mabadiliko kwa wakati mmoja wa miaka mitano huwa ni makubwa sana. Safari hii mpaka sasa hivi Mheshimiwa Rais ni asilimia 61.1 mpaka sasa ya Wabunge wapya. Ahsanteni sana mnaweza kukaa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hiyo inatoa picha kwamba kukaa hapa ni shughuli, kuendelea kuwepo hapa siyo masihara. Inabidi mumsikilize Mheshimiwa Rais na mzingatie atakayoyaeleza hapa unaweza ukarudi, ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 91(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Bunge Kanuni ya 32 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 ningependa kuwajulisha kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yupo pamoja nasi leo hii ili kulihutubia na kulifungua rasmi Bunge jipya la Kumi na Mbili ambalo limekaa katika Mkutano wake wa Kwanza ulioanza tarehe 10 Novemba na tumefanya kazi ya kuwaapisha Wabunge wote 359 hadi hivi sasa, tumefanya kazi ya uchaguzi wa kumpata Spika, tumefanya kazi ya kumpata Naibu Spika na tumefanya kazi ya kupiga kura kuthibitisha pendekezo la uteuzi wa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Hizo ndizo kazi zilizopangwa kwa ajili ya Bunge hili la mwanzo na zote tumeshazikamilisha, imebakia sasa hotuba yako Mheshimiwa Rais ambayo ukiimaliza tutakuwa tunaahairisha Bunge hili hadi wakati ambao nitautaja pale mwishoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, kwa heshima na taadhima sasa ningeliomba nikukaribishe uhutubie Bunge hili na kupitia kuhutubia Bunge hili basi uhutubie Taifa na Taifa zima kwa kweli limejipanga kukusikiliza huko walipo Watanzania na dunia nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, nakukaribisha sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho nilipoingia kwenye ukumbi huu kulifunga Bunge la Kumi na Moja tulibahatika kuwa na Marais wetu wastaafu watatu, lakini kama mnavyokumbuka mmoja wa Marais wetu Wastaafu wa Awamu ya Tatu ametangulia mbele ya haki Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Pia nakumbuka wapo pia baadhi ya Wabunge katika Bunge lililotangulia na watumishi wengine wa Bunge waliotangulia mbele ya haki, basi kwa heshima yao kabla ya kuanza hotuba yangu, ninawasihi sote tusimame tumkumbuke Mheshimiwa Mkapa pamoja na Wabunge wote waliofariki dunia tangu kufungwa kwa Bunge la Kumi na Moja.

*(Hapa Wabunge na Wageni Waalikwa Walisimama kuwaombea watu wote walifariki dunia)*

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Mzee Mkapa pamoja na marehemu wetu wote mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, napenda niseme kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 91(1) imempa dhamana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulifungua rasmi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kwa sababu hiyo nimekuja hapa leo kulihutubia Bunge hili kwa lengo la kutimiza masharti hayo ya Katiba.

Napenda nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujaalia neema ya uhai na kutuwezesha kuiona siku ya leo. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika Job Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuliongoza Bunge hili ukiwa Spika, hongera sana. *(Makofi)*

Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa tena kwa mara nyingine kuwa Naibu Spika tena mara hii akiwa Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la

Mbeya Mjini, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Tulia, huu ni uthibitisho kwamba nchi yetu kupitia Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi inawaamini sana wanawake. Kama mnavyofahamu Makamu wetu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan naye ni mwanamama. *(Makofi/ Vigelegele)*

Aidha, Bunge hili la Kumi na Mbili nalo lina Wabunge wengi wanawake kama ulivyotaja. Kwa msingi huo, napenda nitumie fursa hii kuwaahidi kuwa Serikali ninayoiongoza itaendelea kuwaamini wanawake katika kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Wanawake na akina mama oyee. *(Makofi)*

**WABUNGE WANAWAKE:** Oyee.

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili. Mmechaguliwa kwa vile wananchi wana imani kuwa mna uwezo wa kuwawakilisha vizuri. Nafahamu michakato ilivyokuwa, Wajumbe na kadhalika. Hivyo, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge msiwaangushe wananchi waliowachagua, Watanzania wana imani kubwa sana na Bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi/Kicheko)*

Nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuridhia na kumpitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuja kulizindua Bunge hili baada ya nchi yetu kufanikiwa kumaliza Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kwa uwazi, amani na utulivu mkubwa. Kwa msingi huo, napenda nirudie kuipongeza Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi kwa kusimamia vizuri zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kuanzia uandikishaji wapiga kura, uchukuaji na urejeshaji fomu za wagombea, usimamizi wa kampeni na pia zoezi la kupiga

kura na utoaji wa matokeo mapema. Kwa hakika, tumethibitisha uwezo mkubwa katika kusimamia uchaguzi bila kutegemea misaada kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, Makamu Mwenyekiti wa Tume Jaji Mstaafu Hamid Mahamoud, Makamishna wa Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi Dkt. Wilson Mahera pamoja na watendaji wote wa Tume, hongereni sana kwa kazi nzuri mliyofanya*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawapongeza kwa jinsi tulivyotumia vizuri fedha mlizotengewa, kama inavyofahamika uchaguzi wa mwaka huu uligharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 331 kilitengwa. Hata hivyo mpaka uchaguzi umekamilika, Tume imetumia shilingi bilioni 262 tu. Hii ni ishara nzuri ya uadilifu mkubwa walionao viongozi na watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hongereni sana. Natoa rai kwa taasisi nyingine kuiga mfano mzuri wa Tume hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati kabisa narudia kuwashukuru viongozi wetu wa dini kwa kutuongoza vyema kwa sala na dua katika kipindi chote cha uchaguzi na hatimaye tumeweza kumaliza uchaguzi wetu salama. Nawasihi waendelee kuliombea Taifa letu ili libaki katika mikono ya Mwenyezi Mungu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia pia kuvishukuru vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kusimamia vizuri amani na utulivu wa nchi yetu na mipaka yetu wakati wote wa uchaguzi. Hii ni ishara kuwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ni imara na vinafanya kazi kwa weledi mkubwa, hongereni sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa natoa shukrani nyingi kwa Watanzania wenzangu wote kwa kushiriki vizuri na kuonesha utulivu mkubwa kwenye uchaguzi uliopita kuanzia kwenye zoezi la uandikishaji wapiga kura, wakati wa kampeni, upigaji kura na kupokea matokeo.

Hakuna shaka, uchaguzi wa mwaka huu kwa mara nyingine umethibitisha ulimwengu kuwa sisi watanzania ni wapenda amani, tunajitambua, hatudanganyiki na tumekomaa kidemokrasia, ahsanteni sana Watanzania wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala yote muhimu tuliyoyapanga kuyatekeleza kwenye miaka mitano ijayo tumeyaweka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025 ambayo ina kurasa 303, kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wengi wa Bunge hili wanaifahamu vizuri Ilani hiyo kwa vile wameitumia katika kuomba kura kwa wananchi kwenye Uchaguzi Mkuu uliomalizika. Lakini sambamba na masuala hayo yaliyopo kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi wa mwaka 2020/2025 tunaendelea pia kutekeleza na kusimamia mambo yote niliyoyaeleza wakati nikizundua Bunge la Kumi na Moja tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, kama mtakavyokumbuka kwenye hotuba hiyo ya kuzindua Bunge la Kumi na Moja nilieleza mambo mengi sana ambayo kimsingi yaliyotoa falsafa bila na vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano baadhi tumeyatekeleza vizuri yapo ambayo hatujayatekeleza kwa ukamilifu na mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa hiyo, kwenye miaka mitano ijayo tutaendelea kusimamia na kutekeleza mambo yote niliyoyaeleza kwenye hotuba ya kuzindua Bunge la Kumi na Moja, hii ndiyo sababu nimeamua kuigawa tena hotuba yangu ya uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja kwenu Waheshimiwa Wabunge ili mkaisome na hatimaye ikawaongoze katika kutekeleza majukumu yenu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote naomba Mheshimiwa Spika uniruhusu nitaje baadhi ya mambo muhimu tunayoyapa kipaumbele kikubwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza na muhimu tutakalolipa kipaumbele kikubwa kwenye miaka mitano ijayo

ni kuendelea kulinda na kudumisha tunu za Taifa letu yaani amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Muungano na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Katika hilo naahidi kushirikiana kwa karibu sana na Rais mpya wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. Kamwe hatutakuwa na mzaha na yeyote mwenye kutaka kuhatarisha amani ya nchi yetu, mwenye nia ya kuvuruga umoja na mshikamano wetu na pia mwenye kutaka kutishia uhuru wetu, Muungano pamoja na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kwamba kwenye miaka mitano ijayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatoa ushirikiano mkubwa wa kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa kifupi naweza kusema tutafanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kuleta maendeleo kwa pande zetu zote mbili za Muungano. Katika hilo nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kwa hotuba nzuri aliyoitoa wakati wa kuzindua Baraza la Wawakilishi, kwenye hotuba yake alitoa dira, mwelekeo na kutaja vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Nane ya Zanzibar, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Mwinyi kwa hotuba nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili napenda nimuahidi Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kuwa nitampa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza yote aliyoyaahidi wakati wa uzinduzi rasmi la Baraza la Wawakilishi. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na kulinda na kudumisha tunu za nchi yetu, kwenye miaka mitano ijayo tutaendelea kuimarisha utawala bora hususani kwa kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma pamoja na kuzidisha mapambano dhidi ya rushwa, wizi, ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma. Katika miaka mitano iliyopita tuliwachukulia hatua za kinidhamu watumishi 32,555 na kuiwezesha nchi yetu kushika nafasi ya kwanza kati ya nchi

35 za Afrika kwa kupambana na rushwa kwa mujibu wa *Transparency International* na pia kushika nafasi ya 28 kati ya nchi 136 duniani kwa matumizi mazuri ya fedha za umma kwa mujibu wa utafiti wa Jukwaa la Uchumi la Dunia yaani *World Economic Forum* wa mwaka 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo watumishi wazembe bado wapo, wala rushwa bado wapo na pia wezi na wabadhirifu wa mali za umma bado wapo, kwa hiyo, katika miaka mitano ijayo tutaendelea kushughulikia matatizo hayo, kwa kifupi niseme utumbuaji majipu utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa upande mwingine tutaendelea kuboresha mazingira ya kazi pamoja na maslahi ya watumishi wetu wote ili yaendane na hali halisi ya maisha ya Watanzania, tutaangalia maslahi yao, kwa hiyo watumishi wasiwe na wasiwasi, wachape kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano ijayo pia tumejipanga kuendeleza jitihada za kukuza uchumi, kama unavyofahamu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tulijitahidi kusimamia vizuri uchumi wetu ambapo ulikua kwa wastani wa asilimia saba kwa mwaka. Aidha, pato ghafi la Taifa limeongezeka kutoka shilingi trilioni 94.349 mwaka 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 139.9 mwaka 2019. Tulidhibiti mfumuko wa bei kutoka asilimia 6.1 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 4.4 na kuongeza akiba ya fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani bilioni 4.4 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 5.2 mwezi Julai, 2020 ambazo zinatuwezesha kununua bidhaa na huduma kwa miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo kwenye miaka mitano iliyopita tuliongeza mauzo yetu ya nje kutoka Dola za Marekani bilioni 8.9 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani bilioni 9.7 mwaka 2019, pia kuvutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 14.6 sawa na zaidi ya shilingi trilioni 30. Aidha, tulifanikiwa kupunguza umaskini wa kipato hadi kufikia asilimia 26.4 kwa takwimu za mwaka 2017/2018. Mafanikio haya bila shaka ndiyo yamewezesha mwezi Julai, 2020 nchi yetu kutangazwa kuingia katika kundi la nchi za

uchumi wa kati kutoka kundi la nchi maskini. Hongereni sana Watanzania, hongereni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mafanikio hayo yamepatikana miaka mitano kabla ya muda uliopangwa yaani mwaka 2025, kwa hiyo kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuendeleza mafanikio ya kiuchumi yaliyopatikana na tutahakikisha ukuaji wa uchumi unawanufaisha wananchi hususani kwa kuinua vipato vyao, kupunguza umaskini na tatizo la ajira. Katika hilo tunalenga kukuza uchumi wetu kwa wastani angalau asilimia nane kwa mwaka na pia kutengeneza ajira mpya zipatazo milioni nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kuboresha sera zetu za uchumi jumla na sera za fedha *(microeconomics and monitory policies)* pia kuhakikisha viashiria vyote vya uchumi ikiwemo thamani ya sarafu yetu, mfumuko wa bei pamoja na viwango vya riba vinabaki kwenye hali ya utulivu, pia tutaongeza jitihada za kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba ama yenye riba nafuu ikiwemo mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kupitia mifuko na programu mbalimbali zilizoanzishwa na Serikali ambayo kwa idadi zipo 18 baadhi ya mifuko hiyo ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (*YDF)*, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF)*, Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali *(NEDF)*, Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*SELF-Microfinance Fund)*, Mfuko wa Kuthamini Mikopo ya Mauzo ya Nje, Mfuko wa Kilimo Kwanza na kadhalika. Tutaimarisha usimamizi wa mifuko hii na kuhakikisha Watanzania wanaifahamu, najua mifuko hii ni mingi ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, hivyo basi nakuagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ikawe kazi yako ya kwanza kushughulikia. Ikiwezekana muangalie uwezekano wa kuiunganisha baadhi ya mifuko ili ifanye kazi kwa tija zaidi na kupunguza gharama za uendeshaji. *(Makofi)*

Nataka mifuko hii ikawasaidie wananchi wa kawaida wakiwemo wamachinga, akina baba na akina mama lishe pamoja na wajasiriamali wengine wadogo wadogo, kwa hiyo kazi yako Mheshimiwa Waziri Mkuu ukaanze na hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutoa mikopo tutaendelea pia kutekeleza programu mbalimbali za kukuza ujuzi na maarifa ikiwemo maarifa ya ujasiriamali ili kuwapa ujuzi na uzoefu wananchi wetu utakaowawezesha kujiajiri ama kuajirika ndani na nje ya nchi, tutaendelea pia kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili tuliouzindua mwezi Februari, 2020 ambao utagharimu takribani shilingi trilioni 2.032. Tutahakikisha fedha hizo zinawafikia walengwa ambao ni wananchi maskini.

Mheshimiwa Spika, muhumu zaidi ni kwamba katika kipindi cha miaka mitano ijayo sekta binafsi pia itapewa umuhimu wa pekee sana. Tunataka mtu yeyote atakayetaka kuwekeza asisumbuliwe kwa kuwekewa vikwazo vya aina yoyote. Watanzania ni matajiri, lakini baadhi yao wanasita kuwekeza hapa nchini kwa kuogopa kusumbuliwa na maswali yasiyo na msingi, tunahitaji kuwa na mabilionea wengi wa Kitanzania. *(Makofi)*

Tunahitaji mabilionea wengi wa Kitanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Nataka Watanzania wote washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao sambamba na kuwekeza, Watanzania wahamasishwe kuweka fedha kwenye benki za hapa nchini ili kusaidia benki zetu kufanya biashara na kuimarisha mzunguko wa fedha na kupunguza riba kwa wakopaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania mnaonisikiliza, wakati wa kufanya mambo bila woga nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge ni sasa, tumechelewa sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano ijayo pia tutafungua milango wa sekta binafsi kufanya majadiliano na

Serikali ili kutafuta muafaka wa migogoro ya kibiashara *(business disputes)* iliyopo kwa faida ya pande zote mbili. Lengo letu ni kuona Tanzania inakuwa mahali pazuri pa kufanya biashara duniani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano iliyopita tumefuta tozo 168 ambapo tozo 114 zilihusu kilimo, mifugo na uvuvi na tozo nyingine 54 zilihusu biashara. Tutaendelea na utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hatua hizo kwa lengo la kukuza uchumi kupambana na umaskini na pia kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira, tunakusudia kwenye miaka mitano ijayo kuweka mkazo mkubwa katika kukuza sekta zetu kuu za uchumi na utazlishaji hususani kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, madini, biashara na utalii. Sekta hizi ndizo zenye kuajiri Watanzania wengi, kwa hiyo, ni wazi tukifanikiwa kuzikuza uchumi wetu utakua kwa kasi na hivyo kupunguza matatizo ya umaskini na ukosefu wa ajira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo kwenye kilimo kwa mfano, tunakusudia kuongeza tija na kukifanya kilimo chetu kuwa ni kilimo cha kibiashara, lengo ni kujihakikishia usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwandani na pia kupata ziada ya kuuza nje. Ili kufanikisha hayo tutahakikisha pembejeo na zana bora za kilimo ikiwemo mbegu, mbolea, viuatilifu, dawa na matrekta vinapatikana kwa uhakika na kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaongeza pia eneo la umwagiliaji kutoka hekta 561,383 hadi hekta milioni 1.2 mwaka 2025, hii itasaidia kupunguza utegemezi kwenye mvua. Tataimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji kwa kushirikiana na taasisi za fedha ikiwemo Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na benki nyingine. Tutashughulikia pia tatizo la upotevu wa mazao *(post harvesting loss)* ikiwemo kwa kukamilisha ujenzi wa vihenge na maghala maeneo mbalimbali nchini ambayo yataongeza uwezo wetu wa kuhifadhi mazao kutoka tani 190,000 za sasa hadi tani 501,000. Takwimu zinaonesha kuwa

kila mwaka nchi yetu inapoteza wastani wa kati ya asilimia 30 na asilimia 40 ya mavuno yake kwa sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhi mazao yetu. Zaidi ya hapo tunakusudia kuanzisha bidhaa mbalimbali za huduma za bima ya kilimo na pia kuingia makubaliano ya kibiashara na nchi walaji na wanunuzi wa mazao ili kupata soko la uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazao ya kimkakati tunayolenga kuyapa kiupaumbele kikubwa katika miaka mitano ijayo ni pamba, korosho, chai, kahawa, tumbaku, mkonge, michikichi, cocoa, alizeti pamoja na miwa, lakini pia mazao ya chakula. Nchi yetu kwa mwaka inaagiza tani zipatazo 800,000 za ngano na kwa ujumla tunatumia wastani wa shilingi trilioni 1.3 kuagiza chakula kutoka nje, hii ni aibu kwa nchi kama Tanzania! Hivyo, basi ni lazima tutafute majawabu ya suala hili na hii ndio ikawe kazi ya kwanza ya Waziri wa Kilimo nitakayemteua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo tutaweka mkazo mkubwa kwenye kilimo cha mazao ya bustani yaani matunda, mbogamboga, maua na viungo ambacho kinakua kwa kasi kubwa nchini, hivi sasa nchi yetu inashika nafasi ya 20 kwa kuzalisha wa wingi mazao hayo duniani na mauzo yetu ya nje yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 412 mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 779 mwaka 2019. Hii ndiyo sababu hatuna budi kukiendeleza kilimo cha mazao hayo na katika hilo napenda kuliarifu Bunge hili kuwa kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kununua ndege moja ya mizigo ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya bustani, lakini pia minofu ya samaki pamoja na nyama. Wakulima wetu ni lazima watajirike na shughuli wanazozifanya. Hivyo basi, Mawaziri wa Kilimo, Biashara, Mambo ya Nje na Mabalozi wajipange vizuri katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo; kama mnavyofahamu nchi yetu inashika nafasi ya pili kwa mifugo mingi Barani Afrika. Tuna ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.3, kondoo milioni 5.65, punda 657,389 lakini pia tuna idadi

kubwa ya kuku, bata, kanga na kadhalika. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba sekta hii bado haijanufaisha vya kutosha. Kwa kuzingatia hilo, kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuikuza sekta ya mifugo ili ichangie ukuaji wa uchumi na kupunguza matatizo ya umaskini na ukosefu wa ajira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepanga kuongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta 2,788,901 za sasa hadi hekta milioni sita. Tunataka wafugaji wetu wasiteswe na mifugo yao, mifugo ni utajiri. Sambamba na hayo, tutahamasisha ufugaji wa kisasa, tutaongeza vituo vya kuzalisha mbegu bora na pia kuongeza uzalishaji wa chakula cha mifugo viwandani kutoka tani 900,000 hadi tani milioni nane. Zaidi ya hapo tutakamilisha ujenzi wa machinjio saba unaoendelea maeneo mbalimbali nchini ambapo kwa pamoja yatakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 6,700 na mbuzi 11,000 kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa machinjio hayo siyo tu utasaidia kupatikana kwa nyama bora inayouzwa hadi kwenye masoko ya kimataifa, bali pia utawezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi. Takwimu zinaonyesha kuwa takribani asilimia 90 ya ngozi inayozalishwa nchini kwa sasa haina ubora unaohitajika kimataifa na kwa sababu hiyo mojawapo ni uchinjaji wa wanyama kienyeji. Kwa hiyo, machinjio yanayojengwa yatapunguza tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuikaribisha sekta binafsi kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza bidhaa za mifugo yaani nyama, ngozi, maziwa, kwato na kadhalika na katika hilo tunaahidi kutoa vivutio maalum kwa watakaoweza kuanzisha viwanda vya aina hiyo na viwanda hivyo vitasaidia kuinua vipato vya wafugaji wetu na pia kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania. Na hapa nataka niweke bayana kuwa watendaji wataokwamisha ujenzi wa viwanda hivyo tutawashughulikia, kwa sababu saa nyingine tunakuwa na mipango mizuri, Watendaji wa chini

wanakwamisha. Ilani ya Uchaguzi sitaki icheleweshwe na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yanayofaa kwa shughuli za uvuvi ikiwemo Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Hali hii inaifanya sekta hii kuwa na nafasi ya kutoa mchango mkubwa kwenye kukuza Pato la Taifa na pia kupambana na umaskini na tatizo la ajira. Hata hivyo, kwa sasa mchango wake bado ni mdogo sana. Hivyo basi, kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuikuza sekta hii ya uvuvi ikiwemo kuimarisha shughuli za uvuvi kwenye Bahari Kuu ambako tumekuwa tukipoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *report* ya Kamati ya Bunge kuhusu shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2018; shughuli za uvuvi kwenye Bahari Kuu zinaweza kuiingizia Serikali mapato ya moja kwa moja ya takribani shilingi bilioni 352.1 kwa mwaka endapo mifumo, usimamizi na udhibiti ingekuwa imara. Samaki wangechakatwa hapa nchini hata hivyo mapato yaliyokuwa yamekusanywa kwa kipindi cha miaka tisa yaani kuanzia 2009 hadi 2017 yalikuwa shilingi bilioni 29.79 tu sawa na shilingi bilioni 3.3 kwa mwaka. Kiwango hiki cha mapato hakikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo sababu tunataka kwenye miaka mitano ijayo kuisimamia vizuri shughuli ya uvuvi wa Bahari Kuu ili Taifa letu linufaike na rasilimali zake kwa kuhusisha sekta binafsi. Kwa bahari nzuri, tayari mwaka huu 2020 tumetunga sheria mpya ya kusimamia na kuendeleza uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, tumepanga kununua meli nane za uvuvi kwa kusihirikiana na Shirika la *IFAD*. Meli hizo nane, nne zitakuwa upande wa Zanzibar na nne zitakuwa upande wa Tanzania Bara. Meli hizi zitashiriki katika uvuvi wa Bahari Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu suala la uvuvi wa Bahari Kuu ni la Muungano, tunakusudia pia kujenga bandari kubwa ya uvuvi itakayotoa ajira zipatazo 30,000 na

tutaendelea kuihamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuchakata samaki.

Sambamba na kusimamia Bahari Kuu, tutakuza shughuli za uvuvi kwenye Maziwa yetu Makuu yaani Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa pamoja na Mito yetu mikubwa, tutahamasisha wavuvi wetu wadogo kujiunga kwenye vikundi ili tuweze kuwapatia mitaji, ujuzi, vifaa na zana za uvuvi, na hali kadhalika tutapitia upya tozo za maeneo mbalimbali ili kuwapunguzia wavuvi kero na kuvutia uwekezaji kwa wavuvi wetu. Tutahamasisha pia watu binafsi kujenga mabwawa na kufuga kisasa kwa kutumia vizimba. Sekta ya uvuvi ni lazima itoe mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu. Wateule wote wa sekta hii ni lazima walisimamie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ndoto kufikiria kwamba tutaweza kukuza uchumi au kupambana na umaskini pamoja na tatizo la ukosefu wa ajira bila kuendeleza nguvu katika kukuza sekta ya viwanda. Duniani kote sekta ya viwanda ndiyo muhimili mkuu wa kukuza uchumi, kupambana na umaskini pamoja na matatizo ya ajira. Kwenye miaka mitano iliyopita tulifanikiwa kujenga viwanda vipya takribani 8,477 ambavyo vilitengeneza ajira zipatazo 480,000 ambapo Mkoa wa Pwani uliongoza kwa kujenga viwanda vingi. Nawapongeza sana uongozi wa Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Hivyo basi, kwenye miaka mitano ijayo tutaendeleza jitihada za kukuza sekta hiyo. Mkazo mkubwa tutauweka kwenye viwanda vyenye kutumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini yaani mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi vyenye kuajiri watu wengi na ambavyo bidhaa zake zinatumika kwa wingi hapa nchini kama vile nguo, bidhaa za ngozi, mafuta ya kula, sukari, saruji na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuvutia uwekezaji kwenye sekta ya viwanda tutaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo kuangalia masuala ya kodi na kuondoa vikwazo na urasimu. Pamekuwepo na urasimu nyingi na kusumbuliwa kwa wawekezaji kwa kuzungushwa zungushwa

na hivyo kuwafanya wakate tamaa. Mimi nataka mwekezaji mwenye fedha zake akija apate kibali ndani ya siku 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hiyo nimeamua suala la uwekezaji ikiwa ni pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kulihamishia kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Ofisi ya Rais ili hao wanaokwamisha nikapambane nao mwenyewe. Lakini zaidi ya hapo, tumepanga kujenga Ukanda na Kongani yaani *clusters* za viwanda kila mkoa kulingana na mazao na maliasili zinazopatikana huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano iliyopita tumepata mafankio makubwa kwenye sekta ya madini. Mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 168 mwaka 2014/2015 hadi shilingi bilioni 527 mwaka 2019/2010. Mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019. Zaidi ya hapo kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, mwaka 2019 sekta ya madini iliongoza kwa kutuingizia fedha nyingi za kigeni Dola za Marekani bilioni 2.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kulipongeza sana Bunge la Kumi na Moja kwa kutoa mchango mkubwa katika kupatikana kwa mafanikio haya ikiwa ni pamoja na kutunga sheria humu Bungeni. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Nina imani kuwa, Bunge hili la Kumi na Mbili litafuata nyayo za Bunge la Kumi na Moja na katika hili napenda niliarifu Bunge hili tukufu kuwa kwenye miaka mitano ijayo tutaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa madini yetu kama tulivyofanya kwa kujenga ukuta wa Mirerani kwa kuimarisha Sheria zetu ili madini yetu yasitoroshwe na Serikali kukoseshwa mapato. Aidha, tunakusudia kuendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wakubwa kwa kuzingatia mfano wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na Kampuni ya

Barrick yaliyowezesha kuundwa kwa Kampuni ya *Twiga Minerals Corporation.*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini mbalimbali ikiwemo dhahabu, almasi, *Tanzanite*, chuma, bati, *nickel, copper* na kadhalika. Lakini aidha tuna gesi za aina mbalimbali kama vile ethane, methane pamoja na helium. Kwa taarifa tulizonazo kwa mfano kwenye gesi ya helium ambayo inapatikana kule Rukwa ni tani nyingi sana zilizoko kule za ujazo zikichimbwa zinatosha ku-*supply* dunia nzima kwa miaka 20. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama zinaweza zikahudumia dunia kwa miaka 20 huu ni utajiri mwingine tulionao sisi Watanzania. Hii ndiyo sababu kila siku nimekuwa nikisema sisi siyo maskini, sisi ni matajiri, nchi yetu ni tajiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu madini, pia kwenye miaka mitano ijayo tutaendelea kuimarisha Shirika letu la Taifa la Madini yaani *STAMICO* ili lishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini kuwawezesha wachimbaji wetu wadogo wadogo ikiwa ni pamojha na kuwatengea maeneo ya uchimbaji, kuwapatia mafunzo mikopo pamoja na vifaa na katika hili natambua kuwa wapo baadhi ya watu wamepewa leseni za utafiti na uchimbaji, lakini hawajazifanyia kazi. Tutazifuta leseni zao na maeneo hayo tutawagawia wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo ni muhimu sana katika kukuza sekta ya madini. Tutaendelea pia kuimarisha masoko ya madini pamoja na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafirishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini. Tunataka madini yachimbwe hapa Tanzania, yachenjuliwe hapa Tanzania, yayeyushwe hapa Tanzania kisha bidhaa za madini zitengenezwe hapa Tanzania na ndipo ziuzwe nje ama watu kutoka nje waje kununua bidhaa za madini hapa nchini. Tutakuwa tumetengeneza uchumi wa kutosha lakini pia tutatengeneza ajira za kutosha kwa Watanzania. Ni imani yetu kuwa kutokana na hatua tulizopanga kuzichukua, sekta

ya madini itaweza kuchangia angalau asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii ni sekta nyingine ambayo tutaipa mkazo mkubwa kwenye miaka mitano ijayo; sekta hii imeajiri takribani watu milioni nne. Kwenye miaka mitano iliyopita ilikuwa ikitoa mchango mkubwa ambao ulikuwa unaridhisha ambapo idadi ya watalii waliotembelea nchi iliongezeka kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi watalii 1,510,151 mwaka 2019. Mapato nayo yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.9 mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019. Nitumie fursa hii kuipongeza Hifadhi yetu ya Taifa ya Serengeti kwa kuchaguliwa kuwa hifadhi bora Barani Afrika kwa mwaka 2020. Kwenye miaka mitano ijayo tumejipanga kuongeza iddai ya watalii hadi kufikia milioni tano mwaka 2025 na mapato kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 za sasa hadi Dola za Marekani bilioni sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua tutakazochukua ni pamoja na kupanua wigo wa vivutio vya utalii ikiwemo kukuza utalii wa mikutano na uwindaji wa wanyamapori, kuimarisha utalii wa fukwe, kujenga miundombinu ya kuwezesha meli za utalii kuzuru nchini na kuongeza kasi ya utangazaji wa vivutio vyetu. Vilevile tutazihamaisha taasisi za watu binafsi kuanzisha ranchi, mashamba na bustani za wanyama kama inavyofanyika nchi zingine ili kuzuia ujangili na kukuza utalii, lakini pia kuongeza vipato na fursa za ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo, napenda kuwaarifu Watanzania kupitia Bunge hili tukufu kuwa tumepunguza bei kwa ajili ya kupata wanyama wa mbegu kutoka porini. Mathalani, bei ya nyati wa mbegu imepungua kutoka Dola za Marekani 1,900 hadi kufikia shilingi 200,000, pofu kutoka Dola za Marekani 1,700 hadi shilingi 310,000, swala kutoka Dola za Marekani 150 hadi shilingi 90,000; hivyo basi, nawasihi Watanzania hata ninyi Waheshimiwa Wabunge popote walipo changamkieni fursa hii ya kuanza kufuga wanyama walioko porini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni fursa pekee, kuna nchi mbalimbali zimekuwa zikifanya hivyo, mojawapo ni nchi kama Afrika ya Kusini na kadhalika. Hii itatufanya Watanzania wote tufaidike na biashara ya wanyamapori, lakini pia watu wataanzisha *butcher* za wanyamapori na wataanza kuwala badala ya kula nyama ya pori kuonekana ni adui. Zaidi ya hapo, tutaendelea kupitia upya kodi na tozo mbalimbali ili kuzifuta ama kupunguza kodi zenye kero. Kwenye miaka mitano iliyopita, tulipunguza ada za leseni za biashara ya utalii kwa Wakala wa Kusafirisha Watalii yenye idadi ya magari chini ya manne kutoka Dola za Kimarekani 2,000 hadi Dola za Marekani 500 na matokeo yake idadi ya kampuni za Kitanzania zimeongezeka kutoka 643 mwaka 2015 hadi kampuni 1,687 mwaka 2020. Tutaendelea na hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna imani, hatua hizi nilizoeleza zitatuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea ya kukuza uchumi kwa angalau asilimia nane kwa mwaka na kuinua vipato vya Watanzania, kupunguza umaskini na kutengeneza ajira mpya milioni nane. Hata hivyo, najua ili kufikia malengo haya tunategemea sana kupata ushirikiano kutoka sekta binafsi. Kama mnavyofahamu, sekta binafsi ndiyo *engine* ya kujenga uchumi wa kisasa. Hivyo basi, narudia kuikaribisha sekta binafsi ya hapa nchini na kutoka nje kuwekeza katika sekta nilizozitaja na ambazo sikuzitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia watu wa sekta binafsi kuwa Tanzania ni mahali pazuri na sahihi pa kuwekeza. Nchi yetu ina amani na utulivu, tumebarikiwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji, nchi yetu ipo kwenye eneo la kimkakati, sisi pia ni wanachama wa *East Africa Community* na *SADC* ambazo zina soko la watu takriban milioni 500. Kwa hiyo narudia, kuikaribisha sekta binafsi kuwekeza hapa nchini. Kwa bahati nzuri, tangu mwaka jana tumeanza kutetekeleza Mpango wetu wa Kuboresha Mazingira ya Biashara *(Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment in Tanzania).* Hivyo basi, mazingira ya biashara na uwekezaji, kwenye miaka mitano ijayo yanatarajiwa kuwa bora zaidi kuliko miaka mingine yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi pamoja na sekta ya uzalishaji ni lazima tuimarishe miundombinu, hususan ya usafiri na nishati ya umeme. Kamwe huwezi kukuza sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, uchimbaji madini na utalii bila kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri pamoja na upatikanaji wa huduma za umeme. Kwa hiyo, kama ilivyokuwa kwenye miaka mitano iliyopita, tutaendelea kuweka mkazo mkubwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya usafiri na kuboresha huduma za usafirishaji. Tutakamilisha miradi tuliyoianzisha na kuanza kutekeleza miradi mipya na katika hilo tumepanga kwenye miaka mitano ijayo, kukamilisha ujenzi wa kilometa 2,500 za barabara za lami na kuanza ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 6,006. *(Makofi)*

Najua Wabunge wengi mmetoa ahadi za barabara kwenye maeneo yenu, ili hatimaye tuweze kufikia lengo letu la kuunganisha mikoa na wilaya zote kwa barabara za lami. Barabara hizo zimetajwa kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi na zingine zinatokana na ahadi tulizotoa katika kipindi cha kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepanga pia kukamilisha ujenzi wa madaraja saba na kuanza madaraja mengine 14 likiwemo Daraja la Kigongo – Busisi, Wami na Pangani. Zaidi ya hapo, tutaendelea kushughulikia tatizo la msongamano wa magari kwenye miji na majiji yetu, hususan Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na hapa Dodoma ambako tumepanga kujenga barabara ya mzunguko ya njia nne yenye urefu wa kilometa 110 ambapo makandarasi wawili tayari wamekwishapatikana na ujenzi utaanza hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa reli, tumepanga kuendelea kuimarisha usafiri wa Reli ya Kati na *TAZARA*. Aidha, tutakamilisha ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam - Morogoro hadi Dodoma na kuanza ujenzi wa vipande vya reli ya Mwanza – Isaka; Makutopora – Tabora; Tabora – Isaka hadi Tabora – Kigoma na Kaliua – Mpanda hadi Kalema. Zaidi ya hapo, tutanunua vichwa vya treni ya

njia kuu 39 na kukarabati 31; tutanunua mabehewa ya mizigo 800 na kukarabati 690 na pia tutanunua mabehewa 37 ya abiria na kukarabati mabehewa 60*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa majini, tumepanga kukamilisha upanuzi wa bandari zetu kuu yaani Dar es Salaam, Bandari ya Tanga na Bandari ya Mtwara pamoja na zilizopo kwenye Maziwa yetu Makuu yaani Victoria, Tanganyika na Nyasa. Tumepanga pia kununua meli mpya ya mizigo kwa ajili ya kutoa huduma katika Bahari ya Hindi. Tutakamilisha ujenzi wa meli mpya, kukarabati meli ya MV Butiama na kuanza ujenzi wa meli ya kubeba mabehewa (*ferry wagon*) Ziwa Victoria. Tutaikarabati MV Liemba na MT Sangara pamoja na kuanza ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na mizigo tani 400 na nyingine kubwa ya kubeba mizigo tani 4,000 kwenye Ziwa Tanganyika*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga, tutajenga kiwanja kipya cha Msalato, kikubwa; tutafanya upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege kumi na moja, vikiwepo vya Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Mtwara na Songea pia kujenga kwa kiwango cha lami njia za kutua na kuruka ndege kwenye viwanja vya Iringa, *Lake Manyara,* Tanga, Musoma, Lindi, Kilwa Masoko, Njombe, Singida Simiyu na kadhalika. Zaidi ya hapo, tutanunua ndege mpya tano, ambapo kama nilivyosema, moja itakuwa ya mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu hii ya usafiri pamoja na uboreshaji wa huduma za usafirishaji sio tu utachochea shughuli za uchumi na uzalishaji, lakini pia itakuwa ni hatua nzuri ya kuelekea kufikia malengo yetu ya kuifanya nchi yetu kuwa lango kuu la biashara kwenye ukanda huu; hivyo kuweza kunufaika na nafasi ya kijiografia. Nchi yetu imezungukwa na nchi takribani nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya nishati, tutaendelea kuimarisha miundombinu ya nishati na pia kuboresha upatikanaji wa huduma za umeme. Katika hilo, tunakusudia kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere litakalozalisha megawati 2,115 na kuanza ujenzi

wa miradi mingine mipya ya umeme wa maji katika eneo la Ruhudji megawati 358; Rumakali megawati 222; Kikonge megawati 300 na pia umeme wa gesi asilia Mtwara megawati 300; Somanga Fungu megawati 330, Kinyerezi III megawati 600, Kinyerezi IV megawati 300; pamoja na miradi mingine midogo midogo. Aidha, tunakusudia kuzalisha umeme megawati 1,100 kwa kutumia nishati jadidifu yaani jua, upepo, na jotoardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepanga pia kukamilisha miradi ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kilovoti 400 wa Singida – Arusha hadi Namanga na Iringa – Mbeya hadi Tunduma ambayo itaunganisha nchi yetu na jirani zetu za Kenya na Zambia. Tutatekeleza mingine ya kuunganisha maeneo muhimu ya nchini kwenye Gridi ya Taifa ikiwemo Kigoma. Kwenye miaka mitano iliyopita, tulitekeleza miradi mingi ya kusafirisha umeme na hivyo kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta; na tukaweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 719 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme pia kwenye miaka mitano ijayo, tumepanga kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijafikishiwa umeme, ambapo idadi yake haizidi vijiji 2,384. Kwa sababu kwenye miaka mitano iliyopita, kwa takwimu za hadi jana tumefikisha umeme kwenye vijiji 9,884 kutoka vijiji 2,018 mwaka 2016. Nchi yetu ina vijiji 12,280. Miradi hii yote ya umeme itakapokamilika sio tu itatuwezesha tuwe na umeme wa kutosha na kufikisha umeme kwenye maeneo yote nchini, bali pia itatufanya tuwe na ziada ya kuweza kuuza nje, pia itatusaidia kupunguza gharama za umeme kuliko gharama za sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, kuhusu nishati, kwenye miaka mitano ijayo, tutaanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo yaani *flagship projects* ya bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga lenye urefu wa kilometa 1,445. Mradi huu ni mkubwa na ni wa kwanza kuwa mkubwa duniani kwa kusafirisha mafuta ambayo yako *heated* kwenye *distance* kubwa ya kilometa 1,444 na kilometa zote 1,115 ni Tanzania, kilometa zingine 300

na kitu zitakuwa nchini Uganda. Mradi wa Kusindika Gesi Asilia *(LNG)* Mkoani Lindi, nao tutahakikisha unaanza kufanya kazi. Zaidi ya hapo, tutaendelea kuhamasisha matumizi ya gesi asilia na gesi ya mitungi majumbani, kwenye taasisi na viwanda na magari ili kupunguza uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia hivi sasa ipo kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yaani *The Fourth Industrial Revoulution*) ambayo yanaongozwa na Sekta ya Mawasiliano *(ICT)*. Shughuli nyingi duniani, kwa sasa zinafanyika kwa kutumia TEHAMA. Hivyo basi, na sisi hatuna budi kuendana na kasi hiyo ya kukua kwa sekta ya mawasiliano. Kwa msingi huo, tumepanga, kwenye miaka mitano ijayo, pamoja na masuala mengine, kufikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu, hususan wilayani. Tutaongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi yaani *broadband* kutoka asilimia 45 ya sasa hadi asilimia 80 mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tumepanga kuongeza watumiaji wa *internet* kutoka asilimia 43 ya sasa hadi asimilia 80 mwaka 2025 na pia kuboresha matumizi ya simu za mkononi ili kupatikana nchi nzima. Zaidi ya hapo, tutatoa vipaumbele kwenye masuala ya utafiti na ubunifu kwenye TEHAMA, tutawatambua na kuwasajili wataalam wote wa TEHAMA; na tunakusudia kuweka anuani za makazi *(postal code)* maeneo mbalimbali nchini. Tutaimarisha pia usalama kwenye masuala ya mawasiliano*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na kukuza huduma za mawasiliano, tunakusudia kuendelea kuboresha huduma za jamii, hususan afya, elimu na maji. Kuhusu afya, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge, kwenye miaka mitano iliyopita tumepata mafanikio makubwa sana , ikiwemo kujenga vituo vya kutolea huduma za afya zaidi ya 1,887; Zahanati 1,198; Vituo vya Afya 487; Hospitali za Wilaya 99; Hospitali za Rufaa Mikoa 10; na Hospitali za Rufaa za Kanda tatu. Vilevile, tumepunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka wastani wa vifo 11,000 kwa mwaka

mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa vifo 3,000 kwa mwaka hivi sasa na tunataka vipungue zaidi. Halikadhalika rufaa ya kupeleka wagonjwa nje zimepungua kwa asilimia 90 baada ya kuimarisha huduma za kibingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, hususan zahanati, vituo vya afya na Hospitali za Wilaya kwenye maeneo ambako hazipo. Tutaimarisha pia upatikanaji wa dawa, vifaa na vitendanishi na kuongeza watumishi wa afya pamoja na kuimarisha Mifuko yetu ya Bima ya Afya ili kufikia lengo la kuwawezesha wananchi wote kupata Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa ugonjwa wa *corona,* mbali na kumtanguliza mbele Mwenyezi Mungu, tiba za asili au tiba mbadala nazo zimesaidia sana. Hivyo basi, kwenye miaka mitano ijayo, tumekusudia kuimarisha Kitengo cha Utafiti wa Tiba Mbadala. Sisi Watanzania hatupaswi kamwe kudharau dawa zetu za asili ama tiba mbadala na kwa sababu hiyo, matibabu na maduka rasmi ya dawa asili yataruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, tutaimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ili kufikia viwango vya kimataifa. Tunataka huduma zote za afya zipatikane hapa hapa nchini, akitaka matibabu ya dawa mbadala au za asili atibiwe hapa hapa, akitaka za hospitall atibiwe hapa hapa ili watu waje watibiwe na ikiwezekana watu kutoka nje waje kutibiwa hapa nchini. Kimsingi, tayari wameanza kuja kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu, tutaendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari bila malipo; tutaongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kuongeza idadi ya wanufaika. Aidha, tutaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu, ikiwemo shule, madarasa, mabweni, maabara, maktaba, ofisi na nyumba za walimu, hosteli pamoja na kumbi za mihadhara. *(Makofi)*

Tutahakikisha tunaendelea kuboresha elimu inayotolewa ili iweze kutoa maarifa na ujuzi wa kutosha kwa wahitimu wetu. Tutahimiza ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati, hususan kwa wanafunzi wa kike ambao tunakusudia kujenga shule moja ya sekondari kwenye kila mkoa kwa ajili ya kufundisha masomo ya sayansi kwa wasichana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaweka pia mkazo mkubwa kwenye elimu ya ufundi na katika hilo, tunalenga kuanzisha vituo mahiri vya mafunzo kwa taasisi za elimu ili kuzalisha vijana wenye uwezo unaohitajika kitaifa, kikanda na kimataifa ambapo kiasi cha Dola za Marekani milioni 75 kimepangwa kutumika. Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itabobea katika TEHAMA; Taasisi ya Teknolojia Mwanza itabobea kwenye masuala ya ngozi; Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kitakachobobea katika taaluma za usafiri wa anga na Chuo cha Ufundi Arusha kitabobea katika nishati jadidifu.

Kuhusu maji; mafanikio makubwa sana yamepatikana kwenye miaka mitano iliyopita. Tumetekeleza miradi ipatayo 1,422 yenye thamani ya takribani shilingi trilioni 2.2. Hii imefanya upatikanaji wa maji safi na salama kuongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 70.1 mwaka 2020 kwa vijijini na kwa mijini kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda nikiri kwamba nilipokuwa kwenye kampeni, moja ya changamoto kubwa niliyoelezwa na wananchi, ilikuwa shida ya maji hususan maeneo ya vijijini. Kwa msingi huo, kwenye miaka mitano ijayo tutajitahidi kuelekeza nguvu zaidi katika kushughulikia suala la maji ikiwemo kuhakikisha kuwa fedha zinazopelekwa vijijini kutekeleza miradi ya maji zinatumika vizuri. Kwa sababu ni kweli fedha nyingine zilizokuwa zinapelekwa vijijini zilikuwa hazitumiki vizuri na miradi ilikuwa haikamiliki. Nataka kuona miradi ya maji inayojengwa inakamilika kwa wakati na pia watendaji wawe wabunifu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. Mito na maziwa yetu yatumike kikamilifu katika kuwafikishia maji wananchi wa maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano ijayo, pia tutaimarisha Mfuko wa Taifa wa Maji ili kuuongezea uwezo wa kifedha wa kutekeleza miradi ya maji. Tutakamilisha pia miradi mikubwa ikiwemo ya miji 28 itakayogharimu shilingi trilioni 1.2. Upo mradi wa maji wa kutoa maji Ziwa Victoria unaogharimu takribani shilingi bilioni 600 na mradi mkubwa wa maji wa Arusha wenye thamani ya shilingi bilioni 520.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwasihi Watanzania kulinda vyanzo vya maji na miundombinu inayojengwa. Nitoe wito pia kwa viongozi wote mkiwemo Waheshimiwa Wabunge, kulifanya suala la kutunza vyanzo vya maji na miundombinu yake kuwa ajenda muhimu katika shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano ijayo tumejipanga pia kuendelea kuimarisha na kukuza uhusiano wetu na nchi mbalimbali kwa kuzingatia sera yetu ya mambo ya nje inayoweka msisitizo wa diplomasia ya kiuchumi. Tutakuza urafiki na ujirani mwema na pia tutashiriki kikamilifu kwenye shughuli za kikanda, kibara na kimataifa hususan kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na nimefurahi kumwona Mbunge anayewakilisha Bunge letu la Afrika Mashariki na pia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC),* Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kushirikiana kwenye shughuli za kulinda amani. Halikadhalika kwenye miaka mitano ijayo tutaendeleza jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia, kulinda uhuru na haki ya wananchi na vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kukumbusha kuwa lengo la demokrasia ni kuleta maendeleo na siyo fujo. Hakuna demokrasia isiyo na mipaka. Aidha, uhuru na haki vinakwenda sambamba na wajibu na hakuna uhuru au haki isiyo na wajibu. Vyote vinakwenda sambamba. Najua nimeeleweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi wakati wa kipindi cha kampeni kwenye miaka mitano ijayo tutaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa wajasiriamali wadogo yaani machinga, mama lishe, babalishe, waendesha bodaboda, bajaji na kadhalika. Kama mnavyofahamu kwenye miaka mitano iliyopita tulianzisha utaratibu wa kutoa vitambulisho maalum kwa wajasiriamali wetu wadogo. Kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuviboresha vitambulisho hivyo ikiwemo kuweka picha na taarifa nyingine muhimu, kama ilivyo kwenye Vitambulisho vya Taifa au *passport. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii itawawezesha wafanyabiashara watakaotumia vitambulisho hivyo kutambulika, ikiwemo kwenye benki na hivyo, kupata mikopo kwa ajili ya kukuza biashara zao. Hii pia itawawezesha wafanyabiashara wetu wadogo wadogo kukua na kutajirika. Hilo ndiyo lengo letu. Tunataka wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wawe wanakua na kutajirika na siyo siku zote wabaki kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano ijayo pia tutakuza sekta ya sanaa, michezo na utamaduni ambayo inakua kwa kasi kubwa hivi sasa. Kama nilivyoahidi wakati wa kampeni, tutaikuza zaidi sekta hii, hususan kwa kuimarisha usimamizi wa masuala ya hatimiliki ili wasanii waweze kunufaika na kazi zao. Ninafarijika kuona kuna wasanii ambao ni Wabunge miongoni mwetu humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutahuisha pia Mfuko wa Utamaduni wa Sanaa ili kuwasaidia wasanii wetu ikiwemo kupata mafunzo na mikopo. Tutaanza pia kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya kuziandaa timu zetu za Taifa. Katika hilo, napenda kutumia fursa hii kuitakia heri timu yetu ya *Taifa Stars* kwenye mechi yao dhidi ya Tunisia baadaye leo, pamoja na mwana masumbwi wetu Hassan Mwakinyo ambaye naye ana pambano leo. Watanzania tunataka ushindi, tumechoka kushindwa shindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma. Viongozi, Wabunge na watumishi wote wa Serikali wenye kustahili kuhamia Dodoma tayari wameshahamia Dodoma. Kwenye miaka mitano ijayo tutakamilisha ujenzi wa ofisi na pia kuendelea na ujenzi wa makazi ya watumishi. Zaidi ya hapo, tutaendelea kutekeleza miradi ya miundombinu ambayo tayari nimeitaja, barabara ya njia nne, uwanja wa ndege wa Msalato na kadhalika. Tutashughulikia suala la upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma. Nataka niwahakikishie Wana-Dodoma wote mkiwepo ninyi Wabunge na sisi wote na Watanzania, suala la maji tutalitatua haraka sana Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ambayo tutayapa kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

(i) Tutafanya uendelezaji na uboreshaji wa makazi ya wananchi ambapo tutahakikisha vifaa vya ujenzi vinapatikana kwa gharama nafuu na mikopo ya ujenzi inapatikana kwa riba nafuu; *(Makofi)*

(ii) Tutashughulikia pia masuala la mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Tutashughulikia masuala ya watu na makundi maalum wakiwemo wazee na watu wenye ulemavu; *(Makofi)*

(iv) Tutaendeleza vita dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya. *(Makofi)*

(v) Tutaimarisha sekta ya misitu na nyuki, ikiwemo kwa kuanzisha viwanda vya mazao ya nyuki ili sekta hiyo itoe mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu. Tutahamasisha pia wafugaji wa nyuki. *(Makofi)*

(vi) Tutahakikisha wamiliki wa magari wanatoa mikataba kwa madereva ili kuipa hadhi inayostahili kazi hiyo na kuchochea shughuli za huduma za usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifurahi jana uliwatambulisha hapa madereva akina mama wanaoendesha malori. Ni matumaini yangu na wewe Mheshimiwa Spika utatoa mfano sasa, utaanza kuendeshwa na dereva mwanamke pamoja na Naibu Spika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo suala la madereva inawezekana hata katika Bunge hili ikatungwa sheria mahususi ya kuwalinda madereva wetu wa nchi hii, kwa sababu tutashughulikia pia kero mbalimbali za wananchi ikiwemo migogoro ya ardhi, mirathi, na kadhalika. Kwenye hili nitawaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtusaidie sana katika maeneo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili napenda pia kuwaagiza viongozi wa Serikali kuanzia ngazi za vijiji, kata, tarafa, wilaya na mikoa, kuhakikisha wanatenga siku maalum ya kukutana na wananchi kwenye maeneo yao ili kusikiliza kero zao na kuzipatia ufumbuzi. Kero nyingine ni nyepesi sana ambazo zinaweza zikatatuliwa hata katika *level* ya vijiji, lakini wakati mwingine zinasubiri mpaka viongozi wa kitaifa wanapopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mambo tuliyoyapanga kuyatekeleza ni mengi sana, kweli ni mengi sana, baadhi nimeyaeleza na yapo mengine mengi ambayo yameelezwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM yenye kurasa 303, lakini kwa sababu ya muda sitaweza kuyaeleza yote. Hivyo, basi nawaagiza Mawaziri nitakaowateua, pamoja na watendaji, kuisoma vizuri ilani yetu, kuielewa na kuitafasiri vizuri ilani hiyo katika sera na mipango kazi ya utekelezaji kwenye Wizara au Taasisi wanazoziongoza ili itakapofika mwaka 2025 tuweze kuitekeleza kikamilifu ilani hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua pia ili kuweza kutekeleza vizuri ilani yetu tutahitaji sana kupata ushirikiano kutoka kwenye Bunge hili. Kama mnavyofahamu, Bunge ni kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi. Kwa hiyo, nina uhakika endapo tutashirikiana vizuri miaka mitano ijayo itakuwa ya

maajabu na mafanikio makubwa kwa nchi yetu. Binafsi sina shaka kwamba Bunge hili litatoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda niweke bayana kuwa ninaposema tunaomba ushirikiano, haimaanishi kwamba tunataka muunge mkono kila kitu, la hasha! Penye kukosoa kosoeni, lakini kwa hoja na kutoa mapendekezo ya namna ya kushughulikia. Tunahitaji *constructive criticism* na siyo kukosoa kwa lengo la kukosoa tu. Katika hilo, kwa upande wetu Serikali tunaahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Bunge hili ili kuliwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutatoa pia ushirikiano kwa mhimili wa Mahakama na nimeshukuru sana Mheshimiwa Jaji Mkuu na Majaji wengine wa Mahakama pamoja na Jaji Mkuu wa upande wa Zanzibar wote wako hapa ili nao waweze kutimiza majukumu yao ya kusimamia haki nchini. Kama mnavyofahamu Mahakama ni muhimu sana katika kuongoza Serikali, ni muhimu katika kujenga maelewano katika jamii, kudumisha amani na usalama, pia kuchochea shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Katiba yetu, mimi ni sehemu ya Bunge hili. Hivyo, basi, kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wageni wetu wote walioungana nasi kwenye tukio hili. Ni vigumu kuwataja wote, lakini pia nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mimi niko pamoja nanyi na kamwe sitawaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa unyenyekevu mkubwa, baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba nimelifungua rasmi Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mungu libariki Bunge letu, Mungu abariki Wabunge wote, Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana. *(Makofi)*

# HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, WAKATI WA KUFUNGUA RASMI BUNGE LA 12 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DODOMA, 13 NOVEMBA, 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

***Mheshimiwa Spika;***
Mara ya mwisho nilipoingia kwenye Ukumbi huu Kulifunga Bunge la 11, tulibahatika kuwa na Marais wetu Wastaafu watatu. Lakini leo, wapo wawili. Mmoja, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, ametangulia mbele za haki. Hivyo basi, kabla ya kuanza hotuba yangu, nawasihi sote tusimame tumkumbuke pamoja na wabunge wote waliofariki dunia tangu kufungwa kwa Bunge la 11. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Mzee Mkapa pamoja na marehemu wetu wote mahali pema peponi. Amina.

***Mheshimiwa Spika;***
Baada ya utangulizi huo, napende niseme kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 91 Ibara ndogo ya kwanza imempa dhamana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulifungua rasmi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kwa sababu hiyo, nimekuja hapa leo kulihutubia Bunge hili kwa lengo la kutimiza masharti hayo ya Kikatiba.

Napenda nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia neema ya uhai na kutuwezesha kuiona siku ya leo. Aidha, nakupongeza wewe, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa kwa kuchaguliwa, kwa mara nyingine, kuliongoza Bunge hili ukiwa Spika. Hongera sana. Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Naibu Spika; tena mara hii akiwa Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Mbeya Mjini. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Tulia. Huu ni uthibitisho kwamba, nchi yetu, kupitia Serikali inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi, inawaamini sana wanawake.

Kama mnavyofahamu, Makamu wetu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, naye ni mwanamama. Aidha, Bunge hili la 12 nalo lina Wabunge wengi wanawake. Kwa msingi huo, napenda nitumie fursa hii kuahidi kuwa, Serikali ninayoingoza, itaendelea kuwaamini wanawake katika kushika nafasi mbalimbali za uongozi. ***Wanawake na akinamama Oyee!!!***

Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Wabunge wa Bunge hili la 12. Mmechaguliwa kwa vile wananchi wana imani kuwa mna uwezo wa kuwawakilisha vizuri. Hivyo basi, nawasihi msiwaangushe wananchi waliowachagua. Watanzania wana imani kubwa sana na Bunge hili.

Nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuridhia na kumpitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni sana.

***Mheshimiwa Spika;***

Nimekuja kulizindua Bunge hili baada ya nchi yetu kufanikiwa kumaliza Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kwa uwazi amani na utulivu mkubwa. Kwa msingi huo, napenda nirudie kuipongeza Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi kwa kusimamia vizuri zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu; kuanzia kwenye uandikishaji wapiga kura; uchukuaji na urejeshaji fomu za wagombea; usimamizi wa kampeni na pia zoezi la kupiga kura na utoaji matokeo mapema. Kwa hakika, Tume imedhihirisha uwezo mkubwa katika kusimamia Uchaguzi bila kutegemea misaada kutoka nje. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage; Makamu Mwenyekiti wa Tume, Jaji Mstaafu Hamid Mahmoud Hamid; Makamishna wa Tume; Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahera pamoja na Watendaji wote wa Tume; hongereni sana kwa kazi nzuri.

Lakini, kwa namna ya pekee, nawapongeza kwa namna mlivyotumia vizuri fedha mlizotengewa. Kama inavyofahamika, Uchaguzi wa Mwaka huu uligharamiwa na

Serikali kwa **asilimia 100**, ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 331** kilitengwa. Hata hivyo, mpaka Uchaguzi umekamilika, Tume imetumia **shilingi bilioni 262** tu. Hii ni ishara ya uadilifu mkubwa walionao Viongozi na Watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hongereni sana. Natoa rai kwa Taasisi nyingine kuiga mfano mzuri wa Tume hii.

Kwa moyo wa dhati kabisa, narudia kuwashukuru Viongozi wetu wa Dini kwa kutuongoza vyema kwa sala na dua katika kipindi chote cha Uchaguzi; na hatimaye tumeweza kumaliza Uchaguzi wetu salama. Nawasihi waendelee kuliombea Taifa letu ili libaki katika mikono ya Mwenyezi Mungu.

Narudia pia kuvishukuru vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kusimamia vizuri amani na utulivu wa nchi yetu na mipaka yake wakati wote wa Uchaguzi. Hii ni ishara kuwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ni imara na vinafanya kazi kwa ueledi mkubwa. Hongera sana kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Kwa namna ya pekee kabisa, natoa shukrani nyingi kwa Watanzania wenzangu wote kwa kushiriki vizuri na kuonesha utulivu mkubwa kwenye Uchaguzi uliopita; kuanzia kwenye zoezi la uandikishaji wapiga kura, wakati wa kampeni, upigaji kura na kupokea matokeo. Hakuna shaka, Uchaguzi wa Mwaka huu, kwa mara nyingine, umeuthibitishia ulimwengu kuwa sisi Watanzania ni wapenda amani, tunajitambua, hatudanganyiki na tumekomaa kidemokrasia. Ahsanteni sana Watanzania wenzangu.

***Mheshimiwa Spika;***

Masuala yote muhimu tuliyopanga kutekeleza kwenye miaka mitano ijayo, tumeyaweka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025 ambayo ina kurasa 303. Kwa bahati nzuri, Waheshimiwa Wabunge wengi wa Bunge hili wanaifahamu vizuri Ilani hiyo kwa vile wameitumia katika kuomba kura kwa wananchi kwenye Uchaguzi Mkuu uliomalizika.

Lakini, sambamba na masuala hayo yaliyomo kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi wa mwaka 2020 - 2025, tutaendelea pia kutekeleza na kusimamia mambo yote niliyoeleza wakati nikizindua Bunge la 11, tarehe 20 Novemba, 2015.

Kama mtakavyokumbuka, kwenye Hotuba hiyo ya kuzindua Bunge la 11 nilieleza mambo mengi sana, ambayo, kimsingi, yalitoa falsafa, dira na vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano. Baadhi tumeyatekeleza vizuri; yapo ambayo hatujayatekeleza kwa ukamilifu na mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa hiyo, kwenye miaka mitano ijayo, tutaendelea kusimamia na kutekeleza mambo yote niliyoyaeleza kwenye Hotuba ya Kuzindua Bunge la 11. Hii ndiyo sababu nimeamua kuigawa tena Hotuba yangu ya Uzinduzi wa Bunge la 11 kwenu Waheshimiwa Wabunge ili mkaisome na hatimaye ikawaongoze katika kutekeleza majukumu yenu vizuri.

Hata hivyo, pamoja na hayo yote, naomba *Mheshimiwa Spika* uniruhusu nitaje baadhi ya mambo muhimu tutakayoyapa kipaumbele kikubwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

***Mheshimiwa Spika;***
Jambo la kwanza na muhimu tutakalolipa kipaumbele kikubwa kwenye miaka mitano ijayo ni kuendelea kulinda na kudumisha tunu za Taifa letu, *yaani* Amani, Umoja na Mshikamano, Uhuru wa Nchi yetu, Muungano na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Na katika hilo, naahidi kushirikiana kwa karibu sana na Rais mpya wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. Kamwe, hatutakuwa na mzaha na yeyote mwenye kutaka kuhatarisha amani ya nchi yetu; mwenye nia ya kuvuruga umoja na mshikamano wetu; na pia mwenye kutaka kutishia Uhuru wetu, Muungano pamoja na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Napenda pia kutumia fursa hii kumwahidi Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kwamba, kwenye miaka mitano ijayo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatoa ushirikiano mkubwa na kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya

Zanzibar. Kwa kifupi, naweza kusema, tutafanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kuleta maendeleo kwa pande zetu zote mbili za Muungano. Na katika hilo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kwa hotuba nzuri aliyoitoa wakati wa kuzindua Baraza la Wawakilishi. Kwenye hotuba yake alitoa dira, mwelekeo na kutaja vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Nane ya Zanzibar. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Mwinyi kwa hotuba nzuri. Kupitia Bunge hili, napenda nimwahidi Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi kuwa, nitampa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza yote aliyoahidi wakati wa Uzinduzi Rasmi wa Baraza la Wawakilishi.

***Mheshimiwa Spika;***

Sambamba na kulinda na kudumisha tunu za nchi yetu, kwenye miaka mitano ijayo, tutaendelea kuimarisha utawala bora, hususan kwa kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma pamoja na kuzidisha mapambana dhidi ya rushwa, wizi, ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma. Kwenye miaka mitano iliyopita, tuliwachukulia hatua za kinidhamu watumishi **32,555** na kuiwezesha nchi yetu kushika nafasi ya kwanza kati ya nchi **35** za Afrika kwa kupambana na rushwa, kwa mujibu wa *Transparency International*; na pia kushika nafasi ya **28** kati ya nchi **136** duniani kwa matumizi mazuri ya fedha za umma kwa mujibu wa Utafiti Jukwaa la Dunia (*World Economic Forum)* wa mwaka 2019.

Hata hivyo, watumishi wazembe bado wapo; wala rushwa bado wapo; na pia wezi na wabadhirifu wa mali ya umma bado wapo. Kwa hiyo, kwenye miaka mitano ijayo, tutaendelea kushughulikia matatizo hayo. Na kwa kifupi, niseme, utumbuaji majipu utaendelea. Hata hivyo, kwa upande mwingine, tutaendelea kuboresha mazingira ya kazi pamoja na maslahi ya watumishi wetu wote ili yaendane na hali halisi ya maisha ya Watanzania. Kwa hiyo, watumishi wasiwe na wasiwasi. Waendelee kuchapa kazi.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwenye miaka mitano ijayo pia, tumejipanga kuendeleza jitihada za kukuza uchumi. Kama unavyofahamu, katika

kipindi cha miaka mitano iliyopita, tulijitahidi kusimamia vizuri uchumi wetu, ambapo ulikua kwa wastani wa **asilimia 7** kwa mwaka. Aidha, Pato ghafi la Taifa limeongezeka kutoka **shilingi trilioni 94.349** mwaka 2015 hadi kufikia **shilingi trilioni 139.9** mwaka 2019; tulidhibiti mfumuko wa bei, kutoka **asilimia 6.1** mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa **asilimia 4.4** na kuongeza akiba ya fedha ya kigeni kutoka **Dola za Marekani bilioni 4.4** hadi kufikia **Dola za Marekani bilioni 5.2** mwezi Julai, 2020 ambazo zinatuwezesha kununua bidhaa na huduma kwa **miezi 6**.

Zaidi ya hapo, kwenye miaka mitano iliyopita, tuliongeza mauzo yetu ya nje kutoka **Dola za Marekani bilioni 8.9** mwaka 2015 hadi **Dola za Marekani bilioni 9.7** mwaka 2019; na pia kuvutia uwekezaji wenye thamani ya **Dola za Marekani bilioni 14.6**, sawa na zaidi ya **shilingi trilioni 30**. Aidha, tulifanikiwa kupunguza umasikini wa kipato hadi kufikia **asilimia 26.4** kwa takwimu za mwaka 2017/2018. Mafanikio haya, bila shaka, ndiyo yamewezesha, mwezi Julai 2020, nchi yetu kutangazwa kuingia kundi la nchi za uchumi wa kati kutoka kundi la nchi masikini. Na mafanikio hayo yamepatikana miaka mitano kabla ya muda uliopangwa, yaani mwaka 2025.

Kwa hiyo, kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuendeleza mafanikio ya kiuchumi yaliyopatikana na tutahakikisha ukuaji uchumi unawanufaisha wananchi, hususan kwa kuinua vipato vyao, kupunguza umasikini na tatizo la ajira. Na katika hilo, tunalenga kukuza uchumi wetu kwa wastani wa angalau **asilimia 8** kwa mwaka na pia kutengeneza ajira mpya zipatazo **milioni 8**. Tutaendelea pia kuboresha sera zetu za uchumi jumla na sera za fedha (yaani *macroeconomic and monetary policies*), na pia kuhakikisha viashiria vyote vya uchumi; ikiwemo thamani ya sarafu yetu, mfumko wa bei pamoja na viwango vya riba; vinabaki kwenye hali ya utulivu.

Tutaongeza pia jitihada za kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba ama yenye riba nafuu, ikiwemo mikopo ya **asilimia 10** inayotolewa na Halmashauri zetu; na pia kupitia Mifuko na Programu

mbalimbali zilizoanzishwa na Serikali, ambayo kwa idadi zipo **18**. Baadhi ya Mifuko hiyo ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF); Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF); Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF); Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund), Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo ya Nje; Mfuko wa Kilimo Kwanza. n.k. Tutaimarisha usimamizi wa Mifuko hii na kuhakikisha Watanzania wanaifahamu.

Najua Mifuko hii mingi ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; hivyo basi, nakuagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii ikawe kazi yako ya kwanza kuishughulikia; ikiwezekana, mwangalie uwezekano wa kuiunganisha baadhi ya mifuko ili ifanye kazi kwa tija zaidi na kupunguza gharama za uendeshaji. Nataka Mifuko hii ikiwasaidie wananchi wa kawaida, wakiwemo machinga, akina baba na mama lishe pamoja na wajasiriamali wengine wadogo.

Sambamba na kutoa mikopo, tutaendelea kutekeleza Program mbalimbali za kukuza ujuzi na maarifa, ikiwemo maarifa ya ujasiriamali, ili kuwapa ujuzi na uzoefu wananchi wetu utakaowawezesha kujiajiri ama kuajirika ndani na nje ya nchi. Tutaendelea pia kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili tuliouzindua mwezi Februari 2020, ambao utagharimu takriban **shilingi trilioni 2.032.** Tutahakikisha fedha hizo zinawafikia walengwa, ambao ni wananchi masikini.

Muhimu zaidi ni kwamba, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, sekta binafsi itapewa umuhimu wa pekee sana. Tunataka mtu yeyote atakayetaka kuwekeza asisumbuliwe kwa kuwekewa vikwazo vya aina yoyote. Watanzania ni matajiri lakini baadhi yao wanasita kuwekeza hapa nchini kwa kuogopa kusumbuliwa na maswali yasiyo na msingi. Tunahitaji kuwa na Mabilionea wengi wa Kitanzania. Nataka Watanzania wote washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao.

Sambamba na kuwekeza, Watanzania wahamasishwe kuweka fedha kwenye Benki za hapa nchini ili kusaidia benki

zetu kufanya biashara na kuimarisha mzunguko wa fedha na kupunguza riba kwa wakopaji. *Waheshimiwa Wabunge na Watanzania mnaonisikiliza*, wakati wa kufanya mambo bila woga ni sasa. Kwenye miaka mitano ijayo pia tutafungua milango kwa sekta binafsi kufanya majadiliano na Serikali ili kutafuta mwafaka ya migogoro ya biashara (*business disputes*) iliyopo kwa faida ya pande zote mbili. Lengo letu ni kuona Tanzania inakuwa mahali pazuri pa kufanya biashara duniani. Kwenye miaka mitano iliyopita, tumefuta tozo **168**, ambapo **114** zilihusu kilimo, mifugo na uvuvi na tozo nyingine **54** za biashara. Tutaendelea na hatua hizo.

***Mheshimiwa Spika;***
Mbali na hatua hizo; kwa lengo la kukuza uchumi, kupambana na umasikini, na pia kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira, tunakusudia, kwenye miaka mitano ijayo, kuweka mkazo mkubwa katika kukuza sekta zetu kuu za uchumi na uzalishaji, hususan kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, madini, biashara na utalii. Sekta hizi ndizo zenye kuajiri Watanzania wengi. Kwa hiyo, ni wazi, tukifanikiwa kuzikuza, uchumi wetu utakua kwa kasi na hivyo kupunguza matatizo ya umasikini na ukosefu wa ajira nchini.

Kwa msingi huo, kwenye **KILIMO**, mathalan, tunakusudia kuongeza tija na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kibiashara. Lengo ni kujihakikishia usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwandani na pia kupata ziada ya kuuza nje. Ili kufanikisha hayo, tutahakikisha pembejeo na zana bora za kilimo, ikiwemo mbegu, mbolea, viatilifu/dawa na matrekta, vinapatikana kwa uhakika na kwa gharama nafuu. Tutaongeza pia eneo la umwagiliaji kutoka hekta **561,383** hadi hekta **milioni 1.2** mwaka 2025 ili kupunguza utegemezi kwenye mvua.

Tutaimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za fedha, ikiwemo Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na benki nyingine. Tutashughulikia pia tatizo la upotevu wa mazao (yaani *post harvest loss*), ikiwemo kwa kukamilisha ujenzi wa vihenge na maghala maeneo mbalimabli nchini ambayo

yataongeza uwezo wetu wa kuhifadhi mazao kutoka **tani 190,000** za sasa hadi **tani 501,000**. Takwimu zinaonesha kuwa, kila mwaka, nchi yetu inapoteza wastani wa kati ya **asilimia 30 - 40** ya mavuno yake kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhi. Zaidi ya hapo, tunakusudia kuanzisha bidhaa mbalimbali za huduma ya Bima ya Kilimo na pia kuingia makubaliano ya kibiashara na nchi walaji na wanunuzi wa mazao ili kupata soko la uhakika.

Mazao ya kimkakati tunayolenga kuyapa kipaumbele kikubwa ni pamba, korosho, chai, kahawa, tumbaku, mkonge, michikichi, *cocoa*, alizeti na *miwa*; lakini pia mazao ya chakula. Nchi yetu kila mwaka inaagiza **tani 800,000** za ngano na kwa ujumla, tunatumia wastani wa **shilingi trilioni 1.3** kuagiza chakula kutoka nje. Hii ni aibu kwa nchi kama Tanzania. Hivyo basi, ni lazima tutafute majawabu ya suala hili. Na hii ndiyo ikawe kazi ya kwanza ya Waziri wa Kilimo nitakayemteua.

Lakini, zaidi ya hapo, tutaweka mkazo mkubwa kwenye kilimo cha mazao ya bustani (matunda, mbogamboga, maua na viungo), ambacho kinakua kwa kasi kubwa nchini. Hivi sasa nchi yetu inashika nafasi ya **20** kwa kuzalisha kwa wingi mazao hayo duniani na mauzo yetu ya nje yameongezeka kutoka **Dola za Marekani milioni 412** mwaka 2015 hadi kufikia **Dola za Marekani milioni 779** mwaka 2018/2019. Hii ndiyo sababu, hatuna budi kukiendeleza kilimo cha mazao hayo. Na katika hilo, napenda kuriafu Bunge hili Tukufu kuwa, kwenye miaka mitano ijayo, tunakusudia kununua ndege moja ya mizigo ili kurahisisha uzafirishaji wa mazao ya bustani, lakini pia minofu ya samaki pamoja na nyama. Wakulima wetu ni lazima watajirike na shughuli wanazozifanya; hivyo basi, Mawaziri wa Kilimo, Biashara, Mambo ya Nje na Mabalozi wajipange vizuri katika hili.

Kwa upande wa **MIFUGO**, kama mnavyofahamu, nchi yetu inashika nafasi ya pili kwa wingi wa mifugo Barani Afrika. Tuna ng'ombe **milioni 33.4**; mbuzi **milioni 21.3**; kondoo **milioni 5.65**; punda **657,389**; lakini pia tuna idadi kubwa ya kuku, bata,

kanga, n.k. Hata hivyo, ukweli ni kwamba, sekta hii bado haijatunufaisha vya kutosha.

Kwa kuzingatia hilo, kwenye miaka mitano ijayo, tunakusudia kuikuza sekta ya mifugo ili ichangie ukuaji uchumi na kupunguza matatizo ya umasikini na ukosefu wa ajira nchini. Tutaongeza maeneo ya ufugaji kutoka **hekta 2,788,901** za sasa hadi **hekta 6,000,000**. Tunataka wafugaji wasiteswe na mifugo yao. Mifugo ni utajiri. Sambamba na hayo, tutahamasisha ufugaji wa kisasa; tutaongeza vituo vya kuzalisha mbegu bora na pia kuongeza uzalishaji wa chakula cha mifugo viwandani kutoka **tani 900,000** hadi **tani milioni 8**.

Zaidi ya hapo, tutakamilisha ujenzi wa machinjio saba unaoendelea maeneo mbalimbali nchini, ambapo, kwa pamoja, zitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **6700** na mbuzi **11,000** kwa siku. Ujenzi wa machinjio hizo sio tu utasaidia kupatikana kwa nyama bora itakayouzwa hadi kwenye masoko ya kimataifa bali pia utawezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi. Takwimu zinaonesha kuwa, takriban **asilimia 90** ya ngozi inayozalishwa nchini kwa sasa haina ubora unaohitajika; na sababu mojawapo ni uchinjaji wanyama kienyeji. Kwa hiyo, machinjio yanayojengwa yatapunguza tatizo hilo.

Nitumie fursa hii, kuikaribisha sekta binafsi kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza bidhaa za mifugo (nyama, ngozi, maziwa, kwato, n.k.). Na katika hilo, tunaahidi kutoa vivutio maalum kwa watakaowekeza kwenye viwanda hivyo ambavyo vitasaidia kuinua vipato vya wafugaji wetu na pia kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania. Na hapa, nataka niweke bayana kuwa, watendaji watakaokwamisha ujenzi wa viwanda hivyo tutawashughulikia.

***Mheshimiwa Spika;***
Nchi yetu pia imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yanayofaa kwa shughuli za uvuvi, ikiwemo Ukanda wa Pwani, Maziwa, mito na mabwawa. Hali hii inafanya sekta hii kuwa na nafasi ya kutoa mchango mkubwa kwenye kukuza Pato la Taifa na pia kupambana na umasikini na tatizo la ajira.

Hata hivyo, kwa sasa, mchango wake bado ni mdogo. Hivyo basi, kwenye miaka mitano ijayo tunakusudia kuikuza sekta hii, ikiwemo kuimarisha shughuli za uvuvi kwenye Bahari Kuu, ambako tumekuwa tukipoteza mapato mengi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Kamati ya Bunge kuhusu Shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu ya Mwaka 2018; shughuli za uvuvi kwenye Bahari Kuu zinaweza kuingizia Serikali mapato ya moja kwa moja ya takriban **shilingi bilioni 352.1** kwa mwaka endapo mifumo ya usimamizi na udhibiti ingekuwa imara na samaki wangechakatwa hapa nchini. Hata hivyo, mapato yaliyokuwa yamekusanywa kwa kipindi cha miaka tisa (2009 hadi 2017) yalikuwa **shilingi bilioni 29.79**, sawa na **shilingi bilioni 3.3** kwa mwaka. Kiwango hiki cha mapato hakikubaliki.

Hii ndiyo sababu, tunataka, kwenye miaka mitano ijayo, kuisimamia vizuri shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu ili Taifa letu linufaike na rasilimali zake, kwa kuhusisha sekta binafsi. Kwa bahati nzuri, tayari, mwaka huu (2020) tumetunga Sheria Mpya ya Kusimamia na Kuendeleza ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, tumepanga kununua Meli **8** za Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika IFAD (**4** upande wa Zanzibar na **4** upande wa Tanzania Bara) ili zishiriki katika uvuvi wa Bahari Kuu. Kama mnavyofahamu, suala la uvuvi wa bahari kuu ni la Muungano. Tunakusudia pia kujenga Bandari kubwa ya Uvuvi itakayotoa ajira zipatazo **30,000**; na tutaendelea kuihamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuchakata samaki.

Sambamba na kusimamia Bahari Kuu, tutakuza shughuli za uvuvi kwenye Maziwa yetu Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa) pamoja na Mito yetu mikubwa. Tutahamasisha wavuvi wetu wadogo kujiunga kwenye vikundi ili tuweze kuwapatia mitaji, ujuzi, vifaa na zana za uvuvi; na halikadhalika tutapitia upya tozo na maeneo mbalimbali ili kuwapunguzia wavuvi kero na kuvutia uwekezaji. Tutahamasisha pia watu binafsi kujenga mabwawa na kufuga kisasa kwa kutumia vizimba. Sekta ya uvuvi ni lazima itoe mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu. Wateule wote wa sekta hii ni lazima walisimamie hili.

***Mheshimiwa Spika;***
Ni ndoto kufikiria kwamba utaweza kukuza uchumi au kupambana na umasikini pamoja na tatizo la ukosefu wa ajira bila kuelekeza nguvu katika kukuza sekta ya viwanda. Duniani kote, sekta ya viwanda ndiyo mhimili mkuu wa kukuza uchumi, kupambana na umasikini pamoja na matatizo ya ajira. Kwenye miaka mitano iliyopita, tulifanikiwa kujenga viwanda vipya takriban **8,477** ambavyo vilitengeneza ajira zipatazo **480,000**, ambapo Mkoa wa Pwani uliongoza kwa kujenga viwanda vingi. Naupongeza sana uongozi wa Mkoa wa Pwani.

Hivyo basi, kwenye miaka mitano ijayo, tutaendeleza jitihada za kukuza sekta hiyo. Mkazo mkubwa tutauweka kwenye viwanda vyenye kutumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini (mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi); vyenye kuajiri watu wengi; na ambavyo bidhaa zake zinatumika kwa wingi hapa nchini (nguo, bidhaa za ngozi, mafuta ya kula, sukari, saruji, n.k.).

Ili kuvutia uwekezaji kwenye sekta ya viwanda, tutaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwemo kuangalia masuala ya kodi na kuondoa vikwazo na urasimu. Pamekuwepo na urasimu mwingi na kusumbuliwa kwa wawekezaji kwa kuzungushwa zungushwa na hivyo kuwafanya wakate tamaa. Mimi nataka mwekezaji mwenye fedha akija apate kibali ndani ya **siku 14**. Kwa sababu hiyo, nimeamua suala la uwekezaji ikiwa ni pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kulihamisha kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Ofisi ya Rais ili hao wanaokwamisha nikapambane nao mimi mwenyewe. Lakini, zaidi ya hapo, tumepanga kujenga Ukanda na Kongani (*clusters*) za viwanda kila mkoa kulingana na mazao na maliasili zinazopatikana.

***Mheshimiwa Spika;***
Kwenye miaka mitano iliyopita tumepata mafanikio makubwa kwenye sekta ya madini. Mapato yameongezeka kutoka **shilingi bilioni 168** mwaka 2014/2015 hadi **shilingi bilioni 527** mwaka 2019/2020. Mchango wa sekta ya madini kwenye

Pato la Taifa umeongezeka kutoka **asilimia 3.4** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 5.2** mwaka 2019. Zaidi ya hapo, kwa mara ya kwanza, katika historia ya nchi yetu, mwaka 2019, sekta ya madini iliongoza kwa kutuingizia fedha nyingi za kigeni, **Dola za Marekani bilioni 2.7**. Nitumie fursa hii kulipongeza Bunge la 11 kwa kutoa mchango mkubwa katika kupatikana kwa mafanikio haya.

Nina imani kuwa Bunge hili la 12 litafuata nyayo za Bunge la 11. Na katika hili, napenda niliarifu Bunge hili Tukufu kuwa, kwenye miaka mitano ijayo, tutaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa madini yetu, (kama tulivyofanya kwa kujenga Ukuta Mirerani) kwa kuimarisha Sheria zetu ili madini yetu yasitoroshwe na Serikali kukoseshwa mapato. Aidha, tunakusudia kuendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wakubwa kwa kuzingatia mfano wa Makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na Kampuni ya Barrick yaliyowezesha kuundwa kwa Kampuni ya *Twiga Minerals Corporation*.

Nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini mbalimbali, ikiwemo dhahabu, almasi, Tanzanite, chuma, bati, nickel, copper, n.k. Aidha, tuna gesi aina mbalimbali, kama vile ethane, helium, ambayo hivi karibuni zimepatikana futi za ujazo bilioni 138 kwenye Ziwa Rukwa, ambazo zinaweza kuhudumia dunia kwa miaka 20. Hii ndiyo sababu, kila siku nimekuwa nikisema, sisi sio masikini; sisi ni matajiri. Nchi yetu ni tajiri sana.

Lakini, kuhusu madini pia, kwenye miaka mitano ijayo pia tutaendelea kuliimarisha Shirika letu la Taifa la Madini (STAMICO) ili lishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini; kuwawezesha wachimbaji wetu wadogo, ikiwa ni pamoja na kuwatengea maeneo ya uchimbaji, kuwapatia mafunzo, mikopo pamoja na vifaa. Na katika natambua kuwa, wapo baadhi ya watu wamepewa leseni za utafiti na uchimbaji lakini hawajazifanyia kazi; tutazifuta leseni zao, na maeneo hayo kuyagawa kwa wachimbaji wengine, hususan wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo ni muhimu sana katika kukuza sekta ya madini.

Tutaendelea pia kuimarisha masoko ya madini pamoja na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini. Tunataka madini yachimbwe hapa Tanzania, yachenjuliwe, yayeyushwe na kisha bidhaa za bidhaa za madini zitengenezwe hapa hapa Tanzania; na ndipo ziuzwe nje ama watu kutoka nje waje kununua bidhaa za madini hapa nchini. Ni imani yetu kuwa, kutokana na hatua tulizopanga kuzichukua sekta ya madini itaweza kuchangia angalau **asilimia 10** ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025.

***Mheshimiwa Spika;***
Utalii ni sekta nyingine ambayo tutaipa mkazo mkubwa kwenye miaka mitano ijayo. Sekta hii imeajiri takriban watu **milioni 4**. Kwenye miaka mitano iliyopita, ilikua kwa kiwango cha kuridhisha, ambapo idadi ya watalii waliotembelea nchini iliongezeka kutoka watalii **1,137,182** mwaka 2015 hadi watalii **1,510,151** mwaka 2019. Mapato nayo yaliongezeka kutoka **Dola za Marekani bilioni 1.9** mwaka 2015 hadi kufikia **Dola za Marekani bilioni 2.6** mwaka 2019. Nitumie fursa hii kuipongeza Hifadhi yetu ya Taifa ya Serengeti kwa kuchaguliwa kuwa Hifadhi Bora Barani Afrika kwa mwaka 2020.

Kwenye miaka mitano ijayo, tumejipanga kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia **milioni 5** mwaka 2025 na mapato kutoka **Dola za Marekani bilioni 2.6** za sasa hadi **Dola za Marekani bilioni 6**. Hatua tutakazochukua ni pamoja na kupanua wigo wa vivutio vya utalii, ikiwemo kukuza utalii wa mikutano na uwindaji wanyamapori; kuimarisha utalii wa fukwe; kujenga miundombinu ya kuwezesha meli za utalii kuzuru nchini na kuongeza kasi ya utangazaji wa vivutio vyetu.

Vilevile, tutazihamaisha taasisi na watu binafsi kuanzisha ranchi, mashamba na bustani za wanyama, kama inavyofanyika nchi nyingine; ili kuzuia ujangili na kukuza utalii; lakini pia kuongeza vipato na fursa za ajira kwa Watanzania. Na katika hilo, napenda kuwaarifu Watanzania, kupitia Bunge hili Tukufu kuwa, tumepunguza bei kwa ajili ya kupata wanyama wa mbegu. Mathalan, bei ya nyati wa mbegu

imepungua kutoka **Dola za Marekani 1,900** hadi kufikia **shilingi laki mbili**; Pofu kutoka **Dola za Marekani 1,700** hadi **shilingi 310,000** na Swala kutoka **Dola za Marekani 150** hadi **shilingi 90,000**. Hivyo basi, nawasihi Watanzania wenzangu, popote walipo, kuchangamkia fursa hiyo; ambayo itachochea pia uanzishaji wa *butcher* za wanyama pori.

Zaidi ya hapo, tutaendelea kupitia upya kodi na tozo mbalimbali ili kuzifuta ama kupunguza kodi zenye kero. Kwenye miaka mitano iliyopita, tulipunguza ada ya leseni ya biashara ya utalii kwa wakala wa kusafirisha watalii yenye idadi ya magari chini ya manne kutoka **Dola za Kimarekani 2,000** hadi **Dola za Marekani 500** na matokeo yake idadi ya kampuni za Kitanzania zimeongezeka kutoka **643** mwaka 2015 hadi **1,687** mwaka 2020.

***Mheshimiwa Spika;***
Tuna imani, hatua hizi nilizoeleza zitatuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea ya kukuza uchumi kwa angalau **asilimia 8** kwa mwaka, kuinua vipato vya Watanzania, kupunguza umasikini na kutengeneza ajira mpya **milioni 8.** Hata hivyo, najua, ili kufikia malengo haya, tunategemea sana kupata ushirikiano kutoka sekta binafsi. Kama mnavyofahamu, sekta binafsi ndiyo injini ya kujenga uchumi wa kisasa.

Hivyo basi, narudia kuikaribisha sekta binafsi ya hapa nchini na kutoka nje kuwekeza katika sekta nilizozitaja; na ambazo sikuzitaja. Na napenda niwahakikishie watu wa sekta binafsi kuwa, Tanzania ni mahali pazuri na sahihi pa kuwekeza. Nchi yetu ina amani na utulivu; tumebarikiwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji; nchi yetu ipo kwenye eneo la kimkakati; sisi pia ni Wanachama wa jumuiya mbili, EAC na SADC, ambazo zina soko la watu takriban **milioni 500**.

Kwa hiyo narudia, kuikaribisha sekta binafsi kuwekeza hapa nchini. Na kwa bahati nzuri, tangu mwaka jana, tumeanza kutetekeleza Mpango wetu wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (yaani *Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment in Tanzania*). Hivyo basi,

mazingira ya biashara na uwekezaji, kwenye miaka mitano ijayo, yanatarajiwa kuwa bora zaidi.

***Mheshimiwa Spika;***
Ili kukuza uchumi pamoja na sekta za uzalishaji ni lazima tuimarishe miundombinu, hususan ya usafiri na nishati ya umeme. Kamwe, huwezi kukuza sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, uchimbaji madini na utalii bila kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri pamoja na upatikanaji wa huduma za umeme. Kwa hiyo, kama ilivyokuwa kwenye miaka mitano iliyopita, tutaendelea kuweka mkazo mkubwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya usafiri na kuboresha huduma za usafirishaji. Tutakamilisha miradi tuliyoianzisha na kuanza kutekeleza miradi mipya. Na katika hilo, tumepanga, kwenye miaka mitano ijayo, kukamilisha ujenzi wa **kilometa 2,500** za barabara za lami na kuanza ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa **kilometa 6,006;** ili hatimaye tuweze kufikia lengo letu la kuunganisha mikoa na wilaya zote kwa barabara za lami. Barabara hizo zimetajwa kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi na nyingine zinatokana na ahadi tulizotoa kipindi cha Kampeni. Tumepanga pia kukamilisha ujenzi wa madaraja 7 na kuanza mengine 14, likiwemo Daraja la Kigongo – Busisi, Wami na Pangani.

Zaidi ya hapo, tutaendelea kushughulia tatizo la msongamano wa magari kwenye miji na majiji yetu, hususan Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na hapa Dodoma, ambako tumepanga kujenga barabara ya mzunguko ya njia nne yenye urefu **kilometa 110**; ambapo Wakandarasi wawili tayari wamepatikana na ujenzi utaanza hivi karibuni.

Kwa upande wa usafiri wa reli, tumepanga kuendelea kuimarisha usafiri wa Reli ya Kati na TAZARA. Aidha, tutakamilisha ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam – Dodoma na kuanza ujenzi wa vipande vya reli ya Mwanza – Isaka; Makutopora – Tabora; Tabora – Isaka – Tabora – Kigoma na Kaliua – Mapanda – Kalema. Zaidi ya hapo, tutanunua vichwa vya treni ya njia kuu **39** na kukarabati **31**; tutanunua mabehewa ya mizigo **800** na kukarabati **690**; na pia tutanunua mabehewa **37** ya abiria na kukarabati **60**.

Kuhusu usafiri wa majini, tumepanga kukamilisha upanuzi wa bandari zetu kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na zilizopo kwenye Maziwa yetu Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa). Tumepanga pia kununua meli mpya ya mizigo kwa ajili ya kutoa huduma Bahari ya Hindi. Tutakamilisha ujenzi wa meli mpya, kukarabati meli ya Mv. Butiama na kuanza ujenzi wa meli ya kubeba mabehewa (*ferry wagon*) Ziwa Victoria. Tutaikarabati MV. Liemba na MT. Sangara pamoja na kuanza ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria **600** na mizigo **tani 400**; na nyingine kubwa ya kubeba mizigo **tani 4,000** kwenye Ziwa Tanganyika.

Kuhusu usafiri wa anga, tutajenga kiwanja kipya cha Msalato, tutafanya upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege 11, vikiwemo vya Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Mtwara na Songea na pia kujenga kwa kiwango cha lami njia za kutua na kuruka ndege kwenye viwanja vya Iringa, Lake Manyara, Tanga, Musoma, Lindi, Kilwa Masoko, Njombe, Singida na Simiyu. Zaidi ya hapo, tutanunua ndege mpya tano, ambapo kama nilivyosema, moja itakuwa ya mizigo.

Ujenzi wa miundombinu hii ya usafiri pamoja na uboreshaji wa huduma za usafirishaji sio tu utachochea shughuli za uchumi na uzalishaji lakini pia itakuwa ni hatua nzuri ya kuelekea kufikia malengo yetu ya kuifanya nchi yetu kuwa lango kuu la biashara kwenye Ukanda wetu; na hivyo kuweza kunufaika na nafasi ya kijiografia.

***Mheshimiwa Spika;***

Kuhusu sekta ya nishati, tutaendelea kuimarisha miundombinu ya nishati na pia kuboresha upatikanaji wa huduma za umeme. Na katika hilo, tunakusudia kukamilisha ujenzi wa Bwawa la kufua Umeme la Nyerere litakalozalisha **Megawati 2,115** na kuanza ujenzi wa miradi mingine ya umeme wa maji Ruhudji **Megawati 358**; Rumakali **Megawati 222**; Kikonge **Megawati 300** na pia umeme wa gesi asilia Mtwara **Megawati 300**; Somanga Fungu **Megawati 330**, Kinyerezi III **Megawati 600** na Kinyerezi IV **Megawati 300**; pamoja na miradi mingine midogo midogo. Aidha, tunakusudia kuzalisha umeme

**Megawati 1,100** kwa kutumia nishati jadidifu (jua, upepo, jotoardhi).

Tumepanga pia kukamilisha Miradi wa kusafirisha umeme wa Msongo wa **kilovoti 400** wa Singida – Arusha – Namanga na Iringa – Mbeya – Tunduma ambayo itaunganisha nchi yetu na majirani zetu wa Kenya na Zambia. Tutatekeleza mingine ya kuunganisha maeneo ya humu nchini kwenye Gridi ya Taifa, ikiwemo Kigoma. Kwenye miaka mitano iliyopita, tulitekeleza miradi mingi ya kusafirisha umeme na hivyo kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta; na tukaweza kuokoa kiasi cha **shilingi bilioni 719** kwa mwaka.

Kuhusu umeme pia, kwenye miaka mitano ijayo, tumepanga kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijafikishiwa umeme, ambapo idadi yake haizidi **2,384**. Kwenye miaka mitano iliyopita, kwa takwimu za hadi jana, tumefikisha umeme kwenye vijiji **9,884;** kutoka vijiji **2,018** mwaka 2016. Nchi yetu ina vijiji **12,280**. Miradi hii yote ya umeme itakapokamilika, sio tu itatuwezesha tuwe na umeme wa kutosha na kufikisha umeme kwenye maeneo yote nchini, bali pia itatufanya tuwe na ziada ya kuweza kuuza nje na halikadhalika kupunguza gharama za umeme.

Sambamba na hayo, kuhusu nishati, kwenye miaka mitano ijayo, tutaanza utekelezaji wa Miradi ya kielelezo (*flagship projects*) ya Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga lenye urefu wa **kilometa 1,445** pamoja na Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG) Mkoani Lindi. Zaidi ya hapo, tutaendelea kuhamasisha matumizi ya gesi asilia na gesi ya mitungi majumbani, kwenye taasisi, viwanda na magari ili kupunguza uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.

***Mheshimiwa Spika;***
Dunia hivi sasa ipo kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (yaani *The Fourth Industrial Revoulution*) ambayo yanaongozwa na sekta ya mawasiliano (ICT). Shughuli nyingi duniani, kwa sasa, zinafanyika kwa kutumia TEHAMA. Hivyo basi, sisi nasi hatuna budi kwendana na kasi hiyo ya kukua

kwa sekta ya mawasiliano. Kwa msingi huo, tumepanga, kwenye miaka mitano ijayo, pamoja na masuala mengine, kufikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu, hususan Wilayani, tutaongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi (yaani *broadband*) kutoka a**silimia 45** ya sasa hadi **asilimia 80** mwaka 2025. Aidha, tumepanga kuongeza watumiaji wa *internet* kutoka **asilimia 43** ya sasa hadi **asimilia 80** mwaka 2025 na pia kuboresha matumizi ya simu za mkononi ili kupatikana nchi nzima. Zaidi ya hapo, tutatoa kipaumbele kwenye masuala ya utafiti na ubunifu kwenye TEHAMA; tutawatambua na kuwasajili wataalam wote wa TEHAMA; na tunakusudia kuweka anuani za makazi (*postikodi)* maeneo mbalimbali nchini. Tutaimarisha pia usalama kwenye masuala ya Mawasiliano.

Sambamba na kukuza huduma ya mawasiliano, tunakusudia kuendelea kuboresha huduma za jamii, hususan afya, elimu na maji. Kuhusu **AFYA**, kama unavyofahamu, kwenye miaka mitano iliyopita tumepata mafanikio makubwa, ikiwemo kujenga vituo vya kutolea huduma za afya **1,887** (zahanati **1,198**, vituo vya afya **487,** hospitali za wilaya **99**, Hospitali za Rufaa za Mikoa **10** na Hospitali za Rufaa za Kanda **3).** Vilevile, tumepunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka wastani wa vifo **11,000** kwa mwaka mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa **3,000** hivi sasa na halikadhalika rufaa za kupeleka wagonjwa nje zimepungua kwa **asilimia 90** baada ya kuimarisha huduma za kibingwa.

Kwa msingi huo, kwenye miaka mitano ijayo, tunakusudia kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, hususan zahanati, vituo vya afya na Hospitali za Wilaya kwenye maeneo ambako hazipo. Tutaimarisha pia upatikanaji wa dawa, vifaa na vitendanishi na kuongeza watumishi wa afya pamoja na kuimarisha Mifuko yetu ya Bima ya Afya ili kufikia lengo la kuwawezesha wananchi wote kupata Bima ya Afya. Wakati wa ugonjwa wa *corona*, mbali na kumtunguliza mbele Mwenyezi Mungu, tiba za asili au tiba mbadala nazo zilisaidia sana. Hivyo basi, kwenye miaka mitano, tunakusudia kuimarisha kitengo cha utafiti wa tiba mbadala. Sisi Watanzania hatupaswi kudharau dawa zetu

za asili ama tiba mbadala; na kwa sababu hiyo, matibabu na maduka rasmi ya dawa za asili yataruhusiwa.

Zaidi ya hapo, tutaimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ili kufikia viwango vya kimataifa. Tunataka huduma zote za afya zipatikane hapa nchini; na ikiwezekana watu kutoka nje waje kutibiwa hapa nchini. Na kimsingi, tayari wameanza kuja kutibiwa.

Kwenye **ELIMU**, tutaendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari bila malipo; tutaongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kuongeza idadi ya wanufaika. Aidha, tutaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu, ikiwemo shule, madarasa, mabweni, maabara, maktaba, ofisi na nyumba za walimu, hosteli pamoja na kumbi za mihadhara. Tutahakikisha tunaendelea kuboresha elimu inayotolewa ili iweze kutoa maarifa na ujuzi wa kutosha kwa wahitimu. Tutahimiza ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati, hususan kwa wanafunzi wa kike; ambapo tunakusudia kujenga Shule moja ya Sekondari kwenye kila Mkoa kwa ajili ya kufundisha masomo ya sayansi kwa wasichana. Tutaweka pia mkazo mkubwa kwenye elimu ya ufundi. Na katika hilo, tunalenga kuanzisha vituo mahiri vya mafunzo kwa taasisi za elimu ili kuzalisha vijana wenye uwezo unaohitajika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, ambapo kiasi cha **Dola za Marekani milioni 75** kimepangwa kutumika: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itabobea katika TEHAMA, Taasisi ya Teknolojia Mwanza itabobea kwenye masuala ya Ngozi, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kitakachobobea katika taaluma za usafiri wa anga na Chuo cha Ufundi Arusha kitabobea katika nishati jadidifu.

Kuhusu **MAJI**, mafanikio makubwa sana yamepatikana kwenye miaka mitano iliyopita. Tumetekeleza miradi ipatayo 1422 yenye thamani ya takriban **shilingi trilioni 2.2**. Hii imefanya upatikanaji wa maji safi na salama uongezeke kutoka **asilimia 47** mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 70.1** mwaka 2020 kwa vijijini; na kwa mijini kutoka **asilimia 74** mwaka 2015 hadi **asilimia 84** mwaka 2020.

Hata hivyo, napenda nikiri, nilipokuwa kwenye Kampeni moja ya changamoto kubwa niliyoelezwa na wananchi ilikuwa shida ya maji, hususan maeneo ya vijijini. Kwa msingi huo, kwenye miaka mitano ijayo, tutajitahidi kuelekeza nguvu zaidi katika kushughulikia suala la maji, ikiwemo kwa kuhakikisha fedha zinazopelekwa vijijini kutekeleza miradi ya maji zinatumika vizuri. Nataka kuona miradi ya maji inayojengwa inakamilika kwa wakati. Watendaji wawe wabunifu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. Mito na Maziwa yetu yatumike kikamilifu katika kuwafikisha maji kwa wananchi.

Kwenye miaka mitano ijayo pia, tutaimarisha Mfuko wa Taifa wa Maji ili kuuongezea uwezo wa kifedha wa kutekeleza miradi ya maji. Tutakamilisha pia miradi mikubwa, ukiwemo wa Miji 28 utakaogharimu **shilingi trilioni 1.2**; Mradi wa Maji wa kutoa maji Ziwa Victoria unaogharimu takriban **shilingi bilioni 600** na Mradi Mkubwa wa Arusha wenye thamani ya **shilingi bilioni 520**. Lakini, nitumie fursa hii pia kuwasihi Watanzania kulinda vyanzo vya maji na miundombinu inayojengwa. Na nitoe wito kwa viongozi wote, mkiwemo Waheshimiwa Wabunge, kulifanya suala la kutunza vyanzo vya maji na miundombinu yake kuwa ajenda muhimu katika shughuli zenu.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwenye miaka mitano ijayo, tumejipanga kuendelea kuimarisha na kukuza uhusiano wetu na nchi mbalimbali kwa kuzingatia Sera yetu ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo kwenye diplomasia ya uchumi. Tutakuza urafiki na ujirani mwema na pia tutashiriki kikamilifu kwenye shughuli za Kikanda, Kibara na Kimataifa, hususan kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Tutaendelea pia kushiriki kwenye shughuli za kulinda amani.

Halikadhalika, kwenye miaka mitano ijayo, tutaendeleza jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia, kulinda uhuru na haki za wananchi na vyombo vya habari. Hata hivyo, ningependa kukumbusha kuwa, lengo la demokrasia ni kuleta

maendeleo na sio fujo; na hakuna demokrasia isiyo na mipaka. Aidha, Uhuru na Haki vinakwenda sambamba na wajibu. Hakuna uhuru au haki isiyo na wajibu. Vyote vinakwenda sambamba. Nina uhakika hapo nitakuwa nimeeleweka vizuri.

***Mheshimiwa Spika;***
Kama nilivyoahidi wakati wa kipindi cha Kampeni, kwenye miaka mitano ijayo tutaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa wajasiriamali wadogo (machinga, mama lishe, baba lishe, waendesha boda, bajaji, n.k.). Kama mnavyofahamu, kwenye miaka mitano iliyopita, tulianzisha utaratibu wa kutoa Vitambulisho Maalum kwa wajasiriamali wetu wadogo. Kwenye miaka mitano ijayo, tunakusudia kuviboresha vitambulisho, ikiwemo kuweka picha na taarifa nyingine muhimu, kama ilivyo kwenye Vitambulisho vya Taifa au Pasipoti. Hii itawawezesha wafanyabiashara watakaotumia vitambulisho hivyo kutambulika, ikiwemo kwenye benki na hivyo kupata mikopo kwa ajili ya kukuza biashara. Hii itawawezesha wafanyabiashara wetu wadogo kukua na kutajirika. Na hilo ndilo lengo letu. Tunataka wafanyabiashara wetu wadogo wawe wanakua na kutajirika; na sio siku zote wabaki kuwa wafanyabiashara wadogo.

Kwenye miaka mitano ijayo pia, tutakuza sekta ya sanaa, michezo na utamaduni ambayo inakua kwa kasi kubwa hivi sasa. Kama nilivyoahidi wakati wa Kampeni, tutaikuza zaidi sekta hii, hususan kwa kuimarisha usimamizi wa masuala ya Hati Miliki ili wasaniii waweze kunufaika na kazi zao; tutahuisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwasaidia wasanii wetu, ikiwemo kupata mafunzo na mikopo. Tutaanza pia kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya kuziandaa Timu zetu za Taifa. Na katika hilo, napenda kutumia fursa hii kuitakia heri Timu yetu ya Taifa, *Taifa Stars*, kwenye mechi yao dhidi ya Tunisia baadaye leo pamoja na Mwana Masumbwi wetu, Hassan Mwakinyo, ambaye naye ana pambano leo. Watanzania tunataka ushindi.

***Mheshimiwa Spika;***
Kwenye miaka mitano iliyopita, tumefanikiwa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma. Viongozi na Watumishi wote wa Serikali wenye kustahili kuhamia Dodoma tayari wamehamia. Kwenye miaka mitano ijayo, tutakamilisha ujenzi wa ofisi na pia kuendelea na ujenzi wa makazi ya watumishi. Zaidi ya hapo, tutaendelea kutekeleza miradi ya miundombinu, ambayo tayari nimeitaja (barabara ya njia nne, Uwanja wa ndege wa Msalato) na kushughulikia suala la upatikanaji maji katika Jiji la Dodoma.

Masuala mengine ambayo tutayapa kipaumbele ni kama ifuatavyo:

(i) Uendelezaji na uboreshaji wa makazi wa wananchi, ambapo tutahakikisha vifaa vya ujenzi vinapatikana kwa gharama nafuu na mikopo ya ujenzi inapatikana kwa riba nafuu;

(ii) Tutashughulikia pia masuala ya mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Tutashughulikia masuala ya watu wa makundi maalum, ikiwemo wazee na watu wenye ulemavu;

(iv) Tutaendeleza vita dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya;

(v) Tutaimarisha sekta ya misitu na nyuki, ikiwemo kwa kuanzisha viwanda vya mazao ya nyuki ili sekta hiyo itoe mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu. Tutahamasisha pia ufugaji wa nyuki.

(vi) Tutahakikisha wamiliki wa magari wanatoa mikataba kwa madereva ili kuipa hadhi inayostahili kazi hiyo na kuchochea shughuli za huduma za usafirishaji. Na katika hiyo, ikiwezekana, itatungwa Sheria mahususi.

Tutashughulikia pia kero mbalimbali za wananchi, ikiwemo migogoro ya ardhi, mirathi, n.k. Na katika hili napenda kuwaagiza viongozi wa Serikali kuanzia ngazi za vijiji, kata,

tarafa, wilaya na mikoa kuhakikisha wanatenga siku maalum za kukutana na wananchi kwenye maeneo yao ili kusikiliza kero zao na kuzipatia ufumbuzi.

***Mheshimiwa Spika;***
Kwa ujumla, mambo tuliyopanga kutekeleza ni mengi; ni mengi sana. Baadhi nimeyaeleza na yapo mengine mengi ambayo yameelezwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM yenye kurasa 303, lakini kwa sababu ya muda sitoweza kuyaeleza yote. Hivyo basi, nawaagiza Mawaziri nitakaowateua pamoja na Watendaji kuisoma vizuri, kuielewa na kuitafsri vizuri Ilani hiyo katika Sera na Mipango Kazi ya Utekelezaji kwenye Wizara au Taasisi wanazoziongoza ili ikifika mwaka 2025, tuwe tumeitekeleza yote.

Na katika hilo, ninafahamu kuwa ili kuweza kutekeleza Ilani yetu vizuri, tutahitaji sana kupata ushirikiano kutoka kwenye Bunge hili. Kama mnavyofahamu, Bunge ni kiungo muhimu kati ya Serikali na Wananchi. Kwa hiyo, nina uhakika, endapo tutashirikiana vizuri, miaka mitano ijayo itakuwa ya maajabu na mafanikio makubwa kwa nchi yetu. Na binafsi, sina shaka kwamba, Bunge hili litatoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali.

Hata hivyo, napenda niweke bayana kuwa, ninaposema tunaomba ushirikiano haimaanishi kwamba tunataka muunge mkono kila kitu. La hasha! Penye kukosoa kusoeni; lakini kwa hoja na kutoa mapendekezo ya namna ya kushughulikia. Tunahitaji *constructive criticism* na sio kukosoa kwa lengo la kukosoa tu. Na katika hilo, kwa upande wetu Serikali, tunaahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Bunge hili ili kuliwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo. Tutatoa pia ushirikiano kwa Mhimili wa Mahakama, ili nao uweze kutimiza majukumu yake ya kusimamia haki nchini. Kama mnavyofahamu, Mahakama ni muhimu sana katika kuongoza Serikali. Ni muhimu katika kujenga maelewano katika jamii, kudumisha amani na usalama na pia kuchochea shughuli za kiuchumi.

***Mheshimiwa Spika;***
Kwa mujibu wa Katiba yetu, mimi ni sehemu ya Bunge hili. Hivyo basi, kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wageni wetu wote walioungana nasi kwenye tukio hili. Wageni wapo wengi; hivyo, siwezi kuwataja wote. Napenda nihitimishe kwa kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kuwa mimi nipo pamoja nanyi na wakati wote nitashirikiana na ninyi. Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba nimelifungua rasmi Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Mungu libariki Bunge letu na Wabunge wake!***
***Mungu Ibariki Tanzania!***
**"Ahsanteni sana kwa Kunisikiliza"**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Mheshimiwa Rais, hakika hotuba ambayo umeitoa ni dira kweli kweli kwa miaka mitano ijayo. Nikuhakikishie kwamba kila Mheshimiwa Mbunge amepata nakala na tutaiingiza kwenye *tablets* zetu katika utaratibu wa *soft copy,* itakuwa ni mojawapo ya kiongozi cha shughuli zetu ikiwemo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kufanya kazi za Bunge kwa miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *vision* hii aliyoiweka. Kuongoza ni kuonesha njia Waheshimiwa Wabunge. Sina haja ya kufanya mapitio yoyote, tutafanya Januari au Februari tutakaporudi, kutegemeana na tarehe ya kuahirisha. Mheshimiwa Rais amekuwa muwazi, ameeleza mambo mengi, *vision* yake kwa kweli inatia moyo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais amesema anahitaji mabilionea wengi na kuongoza ni kuonesha njia. Tupeleke *message* hiyo kwa Watanzania. Sisi ndio wawakilishi wao na amesema na ninyi Wabunge kuweni mabilionea pia na amesisitiza maswali maswali ah-ah! Sasa mashaka ya nini tena! *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, kwa ruhusa yako sasa naomba kwa niaba yetu nimteue Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Askofu Gwajima, kwa kifupi sana, atoe shukrani kwa niaba yetu sote. Sijajua vizuri tunavyokaa, aah! Yuko hapa mbele kabisa. Ahsante. Endelea tu. *(Makofi)*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kusema maneno machache kwa niaba ya Wabunge wenzangu. Najua kwamba leo kuna Mabunge mawili humu ndani, uko wewe lakini pia yupo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa sababu hiyo nimezingatia protokali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa *overwhelming* wazungu wanasema. Ni hotuba ambayo akili ya kawaida ya binadamu haiwezi kuibeba *unless* umepata ufunuo kutoka kwa Mungu wa mbinguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hiyo inanisababisha kusema tu shukrani kwako wewe, kwanza nikushukuru sana kwa jinsi ulivyochaguliwa kwa kura nyingi na Bunge hili kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Mbili, pokea kongole za Waheshimiwa Wabunge. *overwhelming*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais pia kwa namna alivyochaguliwa kwa kimbunga cha kura nyingi na akaidhihirishia Tanzania na dunia kwamba mwelekeo wake ni mwelekeo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana kaka yangu na ndugu yangu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, kwa jinsi alivyowageuza kichwa chini, miguu juu wapinzani wake kule Zanzibar na akatudhihirishia kwamba yeye ni nguli na ni jabali na hakika ni daktari si tu wa watu, lakini daktari wa siasa pia, ahsante sana Meshimiwa Dkt. Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hiyo niseme maneno machache ambayo Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Sir Winston Churchill, aliwahi kusema na alisema kwamba; *"If you have a destiny and you stop everywhere throwing stones to the dogs barking at you, you won't arrive at your destiny."* Maana yake ni hii, kwa Wagogo labda hawatanielewa nifafanue; ukiwa unasafiri halafu ukawa unasimama kila mahali kumtupia mawe kila mbwa anayebweka hutafika safari yako. Mheshimiwa Rais wacha mbwa wabweke tuendelee na safari yetu ya kutimiza ilani ya kurasa 303. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wazri Mkuu Winston Churchill alisema, *let them bark for their enjoyment but keep your course.* Maana yake kwamba waache wabweke kwa raha zao, lakini wewe kaza mwendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, lakini pia kwa *projection* hii ya hotuba yako ni muhimu nikiri wazi kwamba hakuna beberu atakayekupenda kwa *projection* hii uliyoipanga kwa nchi yetu. *You have just made a blueprint* katika nchi yetu, kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu, nchi yetu kuweza kujitegemea ku-*finance* uchaguzi wake na kuzuia fedha inayotoka nje, inayotupa masharti ya mambo ya kufuata kinyume na tamaduni zetu za Kiafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais *is a blue print not only for Africa but for the whole world as well.* Umefanya jambo ambalo dunia yote imestaajabu na mabeberu wote umewaacha midomo wazi, ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, umeongea mambo ya ajabu katika hotuba yako. Wakati unazungumza uliposema kwamba utaruhusu maduka yafunguliwe na dawa za kienyeji zianze kuuzwa, Mheshimiwa Nape hapo akawa ananikonyeza ananiambia inawezekana na nyungo za kuruka za wachawi zitaanza kuuzwa, nikamwambia hapana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Rais, nikwambie wewe ni Mwafrika, umetufanya sisi Waafrika dunia yote tusione aibu kusema Rais wetu ni Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Spika anawakaribisha wageni jana hapa, alipowakaribisha wageni wa Mheshimiwa Mpina akasema kwamba najua Wasukuma washamba, kwa hiyo, angalieni msigongwe magari. Lakini sasa Mheshimiwa Spika, nikakumbuka ule usemi wa Mwalimu miaka ya 1978 alipokuwa anasisitiza watu wapanue mashamba. Alipofika hapa Dodoma akawaambia Wagogo panueni mashamba wakashindwa kumuelewa, badala ya kupanua mashamba wakapanua masikio. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika ni mtani wangu jamani, kwa hiyo msiwe na shaka, msiogope. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka niseme kwa dhati sisi Wabunge tulioingia Bungeni kwa mara ya kwanza, pamoja na Wabunge wengine ambao wamekuwepo hapa Bungeni kwa muda mrefu, tunatumia nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Rais. *Performance* yako ya miaka mitano iliyopita imetubeba Wabunge wote kwenye majimbo yetu na bila shaka tumepata kura kupitia wewe. *You just became a beacon of our victory, you became a reference of our victory;* ulikuwa ndiyo tofali la ushindi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu zingine Mheshimiwa Rais hatukuhitaji kupiga kura, tulihitaji kutaja jina lako tu na kura zikapatikana, ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa niaba ya Wabunge wenzangu kwa sababu nimepewa kusema shukrani, nikushukuru sana Mheshimiwa Rais. Niishukuru pia Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi kwa namna ilivyochagua Wabunge wote majabali. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Rais, Wabunge wako wote ni majabali, hakuna Mbunge mnyonge hata mmoja hapa na kwa namna hiyo umejipa urahisi sana wa kutengeneza Serikali yako,

hauhitaji *vetting* kubwa sana, chukua yeyote Mheshimiwa Rais atafanya vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, umewapeleka likizo isiyo na malipo watu wa *vetting* kwa sababu kutoka Kaskazini mpaka Kusini, Mashariki mpaka huko Wabunge wote wanafaa kwa ajili ya kuitumikia Serikali yako na kwenda na mwendo wako Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kwa kusema umetupa heshima kubwa sana, hasa sisi Wabunge ambao ni mara yetu ya kwanza kuingia katika Bunge hili, umetupa heshima kubwa sana na ushindi wako wa kimbunga umeonesha dhahiri kwamba kesho yako inang'aa kuliko jana yako. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, na kwa namna hiyo sasa nikushukuru sana na niseme maneno machache kwamba tufani imekoma katika nchi, sasa ni majira mapya. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge, sitaelekea huko mnakofikiri. *(Makofi/Kicheko)*

Ninataka kumwambia Mheshimiwa Rais tu kwamba kwa kweli Bunge hili la Kumi na Mbili limesheheni watu wa kila aina. Ungekuwa na muda nikupe *demo* kama ya Wabunge ishirini hapa nipigepige tu waongee, basi ungeondoka kidogo hata *tension* nyingine zimepungua, lakini muda wako ni mdogo sana. *(Kicheko)*

Kwa niaba ya Wabunge wote hawa nikushukuru tena Mheshimiwa Rais, na wengi tuna deni kwako, duna deni kwa chama hiki, tuna deni kwa nchi yetu na kwa wananchi wetu. Na wengi ulipita ukisema nileteeni huyu na huyu, na Mama Samia akafanya hivyohivyo, Waziri Mkuu akafanya hivyo hivyo na wengine wote. *(Makofi)*

Jamani wengine tulikuwa hatuchaguliki kabisa, kama Rais asingesema nileteeni fulani, aah! Huko huko. Kwa hiyo,

tuna deni maana ametudhamini kwa wananchi, kwa hiyo, lazima tufanye kazi ya wananchi vizuri, wananchi wafurahi waone kweli Rais aliposema kwamba nileteeni huyu, nileteeni yule kweli iwe ni jambo la namna hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Rais na tukuahidi kuwa kazi itakayofanyika Bunge la Kumi na Mbili ni kazi iliyotukuka kabisa. Tutakuwa *very objective,* na hapa itakuwa ni hoja na zitachambuliwa kwa umakini kwa faida ya nchi yetu tukiongozwa na hotuba hii ambayo umetuwekea siku ya leo bila kumuonea mtu wala nini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa mtakaopata bahati ya kuwa Mawaziri kwa kweli jipangeni, mkidhania kwamba hapa ni *a walkover, you are wrong.* Ili tutekeleze malengo haya ya Mheshimiwa Rais, lazima wote twende na *philosophy* ya Hapa Kazi Tu. Na ninaamini itakuwa hivyo. *(Makofi)*

Basi baada ya maneno hayo, ninaomba tusimame wote ili ndugu zetu wa *Brass Band* waweze kutupatia Wimbo wa Taifa.

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Brass Band ya Jeshi la Polisi ilipiga Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

**SPIKA:** Naomba tukae. Ahsante sana *Brass Band.* Mheshimiwa Rais, tunamalizia tu kwa dakika chache sana, niliahidi kwamba ntatambulisha wageni.

Lakini kabla sijaanza kutambulisha wageni nikukumbushe Katibu wa Bunge, kwenye *register* yako ya majina ya Wabunge, ukumbuke kurekebisha majina ya Waheshimiwa vizuri. Kwa mfano kwenye kampeni za Kawe kule, Mheshimiwa Askofu Gwajima alipewa jina maalum, kule anaitwa Rashid. Kazi imeanza, ahsante sana. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Rais, niombe radhi kwamba wakati tunaanza shughuli hizi wasaidizi wangu hawakuwa wameniletea majina ya baadhi ya wageni wetu maarufu, niombe radhi sana kwa hilo. Lakini sasa nitumie nafasi hii kuwatambulisha rasmi kwamba tunaye mzee wetu, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, miongoni mwetu. Karibu sana baba yetu, tunafarijika sana kuwa nawe miongoni mwetu siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, lakini pia tunaye Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Tunaye pia Makamu wa Rais Mstaafu, Dkt. Mohamed Gharib Bilal. *(Makofi)*

Tunaye pia Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao pia Mawaziri Wakuu Wastaafu, tunaye Mheshimiwa John Samuel Malecela, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, yuko pale. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda. *(Makofi)*

Tunaye Meshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, tunao Maspika Wastaafu, wakiwemo Mheshimiwa Pius Msekwa, tunaye Mheshimiwa Mama Anne Semamba Makinda na tunaye Spika Mstaafu Pandu Ameir Kificho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, wazee hawa tutakuwa nao wiki ijayo waweze kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge kwenye semina zetu za ndani katika kufundana kazi za Ubunge, wajibu wa Mbunge na nafasi yake katika jamii, kwa hiyo, nawakaribisha sana Waheshimiwa Maspika Wastaafu. *(Makofi)*

Kama nilivyowatambulishwa mwanzoni, tunaye Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Martin Ngoga, amefuatana na Wabunge wa Afrika Mashariki popote pale walipokaa naomba wasimame. Ndiyo, iko timu nzima pale, karibu Mheshimiwa Kimbisa, wengine siwezi kuwatambua kwa sababu ni mbali kidogo, lakini namwona Mheshimiwa Makame pale amepiga kanzu, *Engineer* Mnyaa, basi na wengine wote tuliopo. Tunawashukuru sana kwa kufika, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule, Mama Mary Majaliwa. Karibu sana mama yetu. *(Makofi)*

Vile vile yupo Mama Spika, naye yupo. Yuko wapi? Mbona simuoni leo, yuko wapi Mama Spika? Nilitaka Askofu Gwajima akuone. *(Kicheko/Makofi)*

Tunao wake wa Marais na Makamu wa Rais na Mawaziri Wakuu wastaafu, tukiwa na Mama Siti Mwinyi. Ahsante mama. Maryam Mwinyi, mke wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ahsante sana. Tunaye Mama Hasna Kawawa, ahsante mama yetu. Tunaye Regina Lowassa, ahsante mama. Tunaye Mama Tunu Pinda, ahsante sana. Karibuni sana mama zetu, mkiwa pamoja nasi huwa tunafurahi sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa Chama cha Mapinduzi, wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Bara, Mheshimiwa Phillip Mangula. Waheshimiwa, hayo makofi bado hayatoshi. Anaweza akaitisha mafaili yenu upya. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaye, Katibu Mkuu Dkt. Bashiru Kakurwa, tunaye Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar Dkt. Abdullah Sadalla, tunaye Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Ndugu Kheri James, tunaye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma Ndugu Godwin Mkanwa na tunaye Katibu Mkuu Kiongozi Mheshimiwa Balozi *Engineer* John Kijazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama; tunaye Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, tunaye Inspekta Jenerali wa Polisi *(IGP)* Simon Sirro, tunaye Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Diwani Athumani Msuya, tunaye Kamishna Jenerali wa Magereza, Meja Jenerali Suleiman Mzee na tunaye Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakara. Aaaah, Wabunge akina mama, hapo ndiyo penyewe na kigelegele. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Rais, safari moja tulikwenda ya Kibunge Nigeria, sasa pakawa na uchaguzi fulani kwenye *CPA* na Mtanzania mmoja akawa amepata nafasi kubwa na wengine tulikwenda tukiwa wapiga debe. Baada ya yule Mtanzania kuipata ile nafasi basi tukashangilia kwa vigelegele vingi sana, sasa wale Wanaigeria wote wakatutolea macho hivi, tukashangaa ni nini? Kumbe kule kwao vigelegele vinapigwa msibani. Ni hadithi ya kweli kabisa. Tukaacha kuanzia hapo, tukawa makini sana. *(Kicheko)*

Tunaye Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Ndugu John Masunga, tunaye Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungho, tunaye Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndugu James Kaji, tunaye Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Luteni Jenerali Yakub Mohammed na tunaye Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Charles Mbuge. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kuwakaribisha sana Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, tunawahakikishia kwamba Bunge hili litatoa kila aina ya ushirikiano kwa hoja zote zinazoendana na masuala ya vyombo vyetu vya ulinzi

na usalama na tunathamini na kutambua kazi ambayo mnaifanya pamoja na vijana wetu katika majeshi yetu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Watendaji Waandamizi wa Taasisi za Serikali, tunaye Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, *CAG* Vdugu Charles Kichere, karibu sana *CAG.* Pia tunaye Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Ndugu Mathias Kabunduguru, tunaye Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, tunaye Mwenyekiti wa Taifa wa Tume ya Uchaguzi Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage, kana kwamba haitoshi, tunaye Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Charles Mahera. Ndugu Mahera yuko wapi? Yupo eeh? Yupo kule kulia kwangu. Jamani mmemwona Mkurugenzi wa Uchaguzi? *(Makofi/ Kicheko)*

Pia tunaye Gavana wa Benki Kuu, Profesa Florence Luoga. Tunaye Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* - Dkt. Edwin Mhede. Karibu sana. Tunaye Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili, Jaji Mstaafu Harold Nsekela, tunaye Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Ndugu Raya Issa Mselem, karibu sana Raya, tunaye Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Ndugu Xavier Daudi, tunaye Mwenyeji wetu Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge na tunaye Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, *RPC* Gilles Muroto, maarufu sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Mkuu wa Usalama wa Mkoa *(RSO)* - Methuselah Mtonda, karibu sana, tunaye Katibu Tawala *(RAS)* wa Dodoma, Maduka Keissy, karibu sana *RAS,* tuna Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, wakiwakilisha Wakuu wa Wilaya wengine wote - Josephat Maganga; Mkuu wa Wilaya ya Kongwa - Dkt. Suleiman Selela, karibu sana, Mkuu wa Wilaya ya Bahi - Mwanahamisi Munkunda, karibu sana Mwanahamisi. Alikuwa mtumishi wetu hapa Bunge, alikuwa Afisa wetu hapa. Mheshimiwa Rais, ukichukuachukua tena watumishi wangu wawili/watatu, nitashukuru. Wanafanya kazi nzuri huko. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaye Mkuu wa Wilaya ya Kondoa - Fezaria Makota; tunaye Mkuu wa Wilaya ya Chamwino - Vumilia Nyamoga; Mkuu wa Wilaya ya Chemba - Simon Chacha; karibu sana na pia Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa - Jabir Shekimweri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wakurugenzi wa Wilaya za Dodoma kama mpo naomba tu msimame kwa pamoja. Basi huenda wako kwenye kumbi nyingine maana tuna kumbi kadhaa leo. *(Makofi)*

Tunao Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa, *Embassy of the Union of the Comoros,* Balozi Ahmada Badoi Mohammed Faki, ahsante. *Ambassador of the People's Republic of China* - Mama Wang Ke, ahsante sana. *High Commission of the Republic of Namibia, Theresia Samaria. High Commission of The Republic of Mozambique* - Monica Patricio Clemente Musa, ahsante sana. *High Commission of the Republic of Malawi* - Glad Chembemunthali; *High Commission of Pakistan* - Mohammed Salim; *High Commission of the republic of Rwanda - Major General* Charles Karamba; *Embassy of Islamic Republic of Iran* - Hosein Alvadi; Lithiwanian *Honorary Consulate - Sheikh* Alkanabar na Jamaica *Honorary Consulate* - Velissa Elizabeth Delfons. *(Makofi)*

*IMF* tunaye Jens Reinke; *UNDP* - Christine Musisi; *UNDP* - Godfres Mulisa; *UNICEF* - Lawrence Oundu; *Embassy of the Republic of Somalia* - Shena Liban; *Embassy of the Kingdom of Saudi Arabia* - Mohamed Al Ailiani. *(Makofi)*

Watendaji Waandamizi na Wakuu wa Idara za Chama cha Mapinduzi; tunaye Naibu Katibu Mkuu Bara Ndugu Rodrick Mpogoro, Mpogoro alizunguka nchi nzima na Mheshimiwa Rais kwenye kampeni. Natumaini kwenye Majimbo yale yote mlimwona. Ahsante sana. Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Chama cha Mapinduzi, Gaudentia Kabaka; Katibu Mkuu UWT - Queen Mlozi, wale kule. Katibu Mkuu Umoja wa Vijana - Raymond Mangwala; Katibu Mkuu Wazazi - Erasto Sima; Mkuu wa Idara ya Siasa na Uhusiano

wa Kimataifa - Kanali Mstaafu Ngemela Lubinga; Mkuu wa Idara ya Uchumi na Fedha - Dkt. Frank Hawasi; Mkuu wa Idara ya *Organization* - Pereila Silima; Mkuu wa Idara ya Itikadi na Uenezi - Humphrey Polepole. Wakimwona huyo! Alikuwa anawauliza, wataweza kweli?

**WABUNGE FULANI:** Aah wapi.

**SPIKA:** Hata wakiungana! *(Makofi/Vigelegele)*

**WABUNGE FULANI:** Aah wapi.

**SPIKA:** Tunaye Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM - Leila Ngozi; tunao wawakilishi wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu. Wenyeviti na wawakilishi wengine wote wa vyama vingine vyote vya kisiasa. Ahsanteni na karibuni popote pale mlipo. *(Makofi)*

Vilevile tunao viongozi wa dini; tuna Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Sheikh Mustafa Rajab; KKKT Dayosisi ya Dodoma inawakilishwa na Askofu Amon Manaseh Kinyunyu, ahsante ba ba Askofu; BAKWATA Dodoma inaongozwa na Alhaj Sheikh Marusi; Askofu Mkuu *Tanzania Assemblies of God* - Barnabas Mtokambali. Tunaye kiongozi wa dhehebu ya Shia Ithnasheri, Ndugu Azim Dewji. Huyu Azim pamoja na uongozi wa dhehebu hili, basi ngoja niahirishe kidogo. Wenyewe Wabunge wameelewa naongelea nini. Askofu wa Dayosisi ya *Central* Tanganyika, Askofu Dickson Chilongani, ahsante sana baba Askofu, tumefurahi kuwa nawe na tunaye Msaidizi wa Mufti wa Tanzania Sheikh Abubakar Khalid Haji. *(Makofi/ Kicheko)*

Tunaye Mbunge mstaafu wa Bunge letu Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, yule pale, ahsante sana. Huyu katika rekodi zetu, Katibu uje upekue vizuri, nadhani ndiyo Mbunge *longest serving MP,* nadhani kwa sababu yeye amekuwa Mbunge kwa miaka 45 mfululizo! *(Makofi)*

Naomba nimtambulishe Mwenyekiti wa Wazazi Taifa - Dkt. Edmund Bernard Mndolwa. Ahsante sana Mwenyekiti

kwa kuja. Wako Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma, Vyuo Vikuu, Taasisi za Fedha, Wadau wa Vyombo vya Habari na Mawasiliano, Taasisi zisizokuwa za Kiserikali. Kwa kweli nyote wageni wetu karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Saadi Majaliwa, Rehema Kassim Majaliwa Majaliwa, Zuleikha Kassim, Seniya Kachenka na Mwajuma Iddi. Pale mlipo naomba msimame. Karibuni sana. Vilevile tunao viongozi wa CCM kutoka Ruangwa, pale mlipo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wale wageni kutoka Mkoa wa Dodoma, Taasisi mbalimbali za Mkoa wa Dodoma, naomba msimame pale mlipo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika pale mlipo kutoka Mbeya, wengine mko hapa na wageni wote kutoka Chamwino Ikulu karibuni sana. *(Makofi)*

Mwisho, sio kwa umuhimu Mheshimiwa Rais tunao wawakilishi wa madereva akinamama ambao wameingia hapa ukumbuni muda si mrefu. Madereva akinamama naomba msimame. Ahsante sana. Ujumbe wenu mmeusikia toka kwa Mheshimiwa Rais mwenyewe, ametambua kazi yenu na tunawashukuru sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais ameagiza niwe na dereva mwanamama. Hapa Bungeni tuna madereva kama 30 na kitu hivi, katika madereva hao 30, dereva mwanamke ni mmoja tu na kila pakiwa na safari basi kila Afisa anataka kusafiri naye. Sasa Mheshimiwa Rais nikimchukua mimi watalalamika hawa jamaa. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa kweli kuna *imbalance* kubwa ya madereva wanawake kama alivyosema Mheshimiwa Rais, nafikiri Wizara zote, nendeni mkafanye sensa muona. Mtakuwa asilimia 99 kama sio 100 ni wanaume watupu. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais nadhani ni eneo moja la kulitazama na kulirekebisha katika ajira zake. *(Makofi)*

Sasa matangazo madogo madogo tu ya dakika za mwisho ili tuweze kumaliza; Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo tuliambiana, kwanza leo jioni yale mashindano ya mpira wa kikapu ya nchi nzima yanayodhaminiwa na *CRDB* yatafunguliwa na mimi pamoja na ninyi kwenye uwanja wa Chinangali karibu na uwanja wa ndege. Nawaomba sana kuanzia saa 9.00 kadri mtakavyoweza tuwe pamoja. Baada ya hapo saa 12.00 kuelekea saa 1.00 jioni pale *Morena Hotel* kutakuwa na mchaparo ambao umedhaminiwa na wenzetu *CRDB.*

Nawaomba sana mfike kwa sababu wamefanya maandalizi ya kukata na shoka. Nawaombeni sana. Hiyo ni leo, Ijumaa. Usiku saa 4.00 msisahau kuangalia mechi ya Tanzania na Tunisia kama Mheshimiwa Rais alivyotukumbusha, maana sisi Bunge huwa ni washabiki wakubwa sana wa Timu ya Taifa. *(Makofi)*

Kwa kesho sasa Jumamosi, Benki ya *NMB,* imeandaa hafla ya kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, kesho Jumamosi tarehe 14 Novemba katika viwanja vya *PSSSF,* mzidi kuviulizia tu mtavifahamu Waheshimiwa Wabunge wageni. Viwanja vya *PSSSF* Kambarage kuanzia hiyo hiyo 12 jioni. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa sana katika hafla hiyo. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mwenyekiti wa Tawi la Simba Bungeni, anasema kwamba Simba Mjengoni *get together party* itafanyika *Kisasa Town Complex,* kuanzia saa moja jioni siku ya Jumatano tarehe 18 Novemba. Kwa hiyo washabiki wote na wapambe wa Simba wanakaribishwa, lakini pia wale Wabunge ambao ni mashabiki wa Yanga pia mnakaribishwa na hasa tunao wageni wageni kama Mbunge wa Kinondoni, Mbunge wa Newala, Mbunge wa Iramba na wengine wengine, mje muangalie *next level* ni kitu gani! *(Kicheko/Makofi)*

Mwisho kabisa Waheshimiwa Wabunge, niwatakie mwisho wa mwaka mwema. Mtakapokuwa mnaondoka basi muendeshe magari yenu vizuri, taratibu, tukisimamishwa

barabarani, tusimame tuwasikilize matrafiki, tusigombane nao kwa sababu nia yao ni njema. Niwatakie Krismasi njema na kheri ya mwaka mpya. *(Makofi)*

Kwa kuwa bado hatujapata Baraza na Mheshimiwa Waziri Mkuu bado hajaapishwa, lile jukumu la yeye kutoa tarehe na hotuba ya mwisho basi litakuwa haliwezekani na Mheshimiwa Rais hajatuambia anamuapisha lini, lakini hilo ni la kwake hatuwezi kumuuliza hapa. Basi jukumu hilo nitalifanya mimi ambalo huwa ni la kwake, la kututajia tarehe ambayo tutakutana tena. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge msiondoke, huenda Mheshimiwa Rais akatangaza siku ya kumuapisha Mheshimiwa Waziri Mkuu siku yoyote, kwa hiyo tuwepo tuwepo pamoja na hizo semina za wiki ijayo pia ili tuweze kushiriki kule Chamwino. Ni muhimu sana kuwa na Waziri Mkuu wetu wakati Mheshimiwa Rais anapomuapisha.

Kwa hiyo basi, sasa Waheshimiwa Wabunge wala sitawahoji kwa sababu kuwahoji huwa inatakiwa Waziri Mkuu atoe Hoja ya Kuahirisha Bunge sasa leo hakuna hoja iliyotolewa au sio? Kwa hiyo naahirisha moja kwa moja bila kuwahoji, maana nikiwahoji hapa wengine wageni watasema hapana, tuendelee. Mheshimiwa Rais atashangaa hawa wanataka tena wakeshe humu humu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Mkutano huu wa Bunge hadi tarehe 2 Februari, 2021. Ahsante, naomba sasa tusimame. *(Makofi)*

*(Saa 12.08 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 2 Februari, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*